

## Chemical azidi kunoa kichwa
UKURASA 20



## England hatihati kumkosa Alexander-Arnold
UKURASA 21

**MAISHA** Nipashe Baba, Mama na Mwana *Jumapili*



Kisamvu cha nazi



MAISHA NI NYUMBA
Nyumba imara huhimili vishindo vingi



HARUSI



USIJIKANDIKE 'MAKE UP'
**Fuata njia hizi utaonekana mrembo**
UKURASA 9


# Nipashe JUMAPILI
MWANGA WA JAMII
Jumapili Juni 6, 2021 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • No. 0580603
www.ippmedia.com
www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US




RIPOTI MAALUM

# Mtoto kuzaliwa utumbo uko nje

• **Katika** kila 100 wenye tatizo hilo, 90 wapoteza maisha, mikoa inayoongoza yatajwa, mabingwa Muhimbili wajitosa kuokoa... *Endelea ukurasa 4*

## YALIYOMO


**UKURASA WA 2**
**ASKARI UHIFADHI KUSHTAKIWA KIJESHI**
WAZIRI wa Maliasili na Utalii, Dk. Damas Ndumbaro, amesema kesho (Jumatatu) anatarajia...

**UKURASA WA 5**
**WAZIRI APIGA 'STOP' WANANCHI KUUZIWA NGUZO ZA UMEME**
WAZIRI wa Nishati, Dk. Medard Kalemani, amepiga marufuku wananchi kuuziwa nguzo za...


## Serikali yafafanua chanjo ya corona iliyoruhusu
UKURASA 2




Makamu wa Rais, Dk. Philip Isdor Mpango, akionyesha kitabu chenye mpango kabambe wa uhifadhi wa mazingira nchini, baada ya kuuzindua katika maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani, jijini Dodoma jana. **PICHA: OMR**

## Mpango ampatia mtihani Jafo
UKURASA 3


**MICHEZO** **YANGA YAWEKA MIKAKATI MEZANI** UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6

# Serikali yafafanua chanjo ya corona iliyoruhusu nchini

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

SERIKALI imetoa ufafanuzi kuhusu chanjo ya virusi vya corona iliyoruhusiwa kuingia nchini kuwa ni kwa ajili ya raia wa kigeni wanaoihitaji, balozi mbalimbali nchini na wafanyakazi wao.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dodoma jana, Msemaji Mkuu wa Serikali, Gerson Msigwa, alisema serikali imetoa ruhusa kuingizwa kwa chanjo hiyo kwa ajili ya makundi hayo.

Msigwa alisema serikali imetoa ruhusa kwa balozi na mashirika ya kigeni kuingiza chanjo ya ugonjwa wa corona ili kutoa fursa ya kuchanja raia wa kigeni na wafanyakazi ambao baadhi yao wameshindwa kurudi kwao kutokana na masharti yaliyowekwa.

"Serikali imetoa ruhusa kwa balozi mbalimbali kuingiza chanjo za corona nchini ili kuchanja raia wa kigeni pamoja na wafanyakazi wao waliopo nchini ili kuwawezesha kukidhi masharti yaliyowekwa katika mataifa yao," Msigwa alifafanua.

Alisema hali hiyo itasaidia raia mbalimbali wa kigeni kupata chanjo ya corona ili waweze kuwa na sifa za kurudi katika mataifa yao.

"Katika kukabiliana na corona kila taifa limeweka njia zake na hawa wanafanya kazi katika balozi, ni raia wa kigeni ambao wanashindwa kurudi katika mataifa yao kutokana na kutochanjwa chanjo ya corona.

"Kwa hiyo kama tutaendelea kuwanyima kupata huduma hii itakuwa ni uvunjaji wa haki za binadamu," alisema.

Msigwa pia alisema Rais Samia Suluhu Hassan amekabidhiwa mapendekezo ya kamati ya wataalamu wa afya kuhusu chanjo ya corona ambayo yatafanyiwa kazi na Baraza la Mawaziri. "Sasa haya ni mapendekezo ya wataalamu, na Rais ameelekeza mapendekezo haya sasa yaandikiwe andiko na yawasilishwe katika Baraza la Mawaziri ili kujadiliwa na kufanyiwa umuzi na baada ya hapo serikali itakuja na tamko juu mapendekezo hayo. "Lakini kuna balozi na taasisi mbalimbali za kimataifa, hizi zimeruhusiwa kuleta chanjo kwa ajili ya raia wa nchi zao na watumishi wao, na hii ni kwa ajili ya kufanya balozi na taasisi hizi kuendelea na kazi zao kama kawaida kwani bila kufanya hivyo kumekuwa na changamoto," alifafanua.

Katika mkutano huo, Msigwa pia alizungumzia hali ya ukusanyaji wa mapato nchini, akibainisha kuwa imeendelea kuimarika licha ya serikali kuondoa matumizi ya nguvu katika ukusanyaji na wafanyabiashara kulipa kodi kwa hiyari bila kutumika kwa vikosi kazi.

"Kwa hiyo, Watanzania msiwe na hofu, serikali inakusanya kodi kama kawaida kwa ajili ya kuendesha shughuli zake na kutoa huduma kwa wananchi ikiwamo kugharamia mishahara, kuhudumia Deni la Taifa na kugharamia miradi ya maendeleo," alisema.

Alisema Rais Samia pia anaendelea kutekeleza miradi mikubwa ya kimkakati iliyoachwa na mtangulizi wake, Hayati Dk. John Magufuli.

Miradi hiyo ni pamoja na ujenzi wa reli ya kisasa (SGR), bwawa na kufua umeme la Julius Nyerere na ujenzi wa madaraja marefu baharini na Ziwa Victoria.

Vilevile, alisema kuwa hali ya uchumi wa taifa ni nzuri japo yapo madhara ya corona kama ilivyo kwa nchi zingine duniani.

"Uchumi wetu uliokuwa unakua kwa wastani wa asilimia 6.9 umeshuka kidogo hadi wastani wa asilimia 4.7 na matarajio ni kuwa uchumi wetu utaendelea kukua vizuri kutokana na hatua madhubuti ambazo zimechukuliwa," alisema.

Virusi vya corona vilibainika kwa mara ya kwanza Wuhan, China Novemba mwaka juzi na vimesababisha vifo kwa mamilioni ya watu duniani.

# Askari uhifadhi kushtakiwa katika mahakama za kijeshi

**Na Romana Mallya**

WAZIRI wa Maliasili na Utalii, Dk. Damas Ndumbaro, amesema kesho (Jumatatu) anatarajia kusaini kanuni ili kuanzia Julai Mosi, mwaka huu askari pori atakayekiuka miiko yake ya kazi hatapelekwa tena mahakama za kawaida bali za kijeshi na atafukuzwa kazi mara moja.

Ndumbaro aliyasema hayo jana bungeni jijini Dodoma wakati wa kuidhinisha bajeti ya wizara hiyo ya Sh. bilioni 571.6 ambayo ilijadiliwa kwa siku mbili.

Alisema anakwenda kusaini kanuni ili kuhakikisha nidhamu ya askari hao inakaa vizuri na kuondokana na migogoro baina ya wananchi na wahifadhi.

"Chanzo cha migogoro hii na kusababisha wakati mwingine kuwana saa nyingine ni rushwa, askari wetu wanaomba rushwa ili waingie kulima, askari wetu wanaomba rushwa ili wawaruhusu wafugaji waingie, sasa fedha ya rushwa ikiisha anataka aongezewe rushwa ndipo mgogoro unapoanza.

"Wananchi tukatae kutoa rushwa kutoka mwanzo namba yangu na ya mheshimiwa waziri, ya katibu mkuu zipo wazi kwa mtu yeyote kupokea malalamiko yoyote yenye ushahidi ili tuweze kuchukua hatua, ninaamini suala hili sasa linakwenda kupatiwa ufumbuzi wa kudumu," alisema.

Waziri Ndumbaro alisema katika mijadala ya wabunge wameeleza migogoro kati ya wahifadhi na wananchi na wapo waliofariki.

"Wapo wananchi wamefariki na wapo wahifadhi 12 wamefariki roho hizi za Watanzania ni wengi sana, serikali haipendi kuona mwananchi anakufa kwa sababu yoyote na wizara hatufurahishwi na jambo hili, wabunge mmesema hapa wananchi wengi wamefariki kutokana na migogoro kati ya wahifadhi na wananchi, tufike sehemu tuseme sasa inatosha, tutafute ufumbuzi ambao ni wa kwetu wote," alisema.

Alisema wabunge wachukue jukumu la kuelimisha wananchi kwamba maeneo ya uhifadhi wasiingie kufanya shughuli nyingine na wanapokamatwa wasisababishe kufikia kuleta mapigano na kupoteza maisha.

Alisema wizara imeanza kuchukua hatua na tayari askari 61 wamechukuliwa hatua za kufukuzwa kazi, 40 wamesimamishwa kupisha uchunguzi na moja kati ya kazi ya kwanza waliofanya na Naibu Waziri wa wizara hiyo ni kwenda Ifakara kufukuza kazi askari watatu.

"Mkakati wetu ni rahisi sana tukipata malalamiko yenye ushahidi usiokuwa na shaka tunaitisha paredi na kumfukuza askari kwa fedheha kwa sababu hatupendi askari mwenye mafunzo anakiuka miiko ya kazi yake, tunahitaji ushirikiano wa wananchi na wabunge," alisema.

Kuhusu vitalu alikiri ufanyaji kazi umeshuka huku akitaja sababu kuwa ni baadhi ya nchi kuweka zuio, Marekani waliweka na kufungua na sasa nchi za Umoja wa Ulaya sasa wanalifanyia kazi.

Kuhusu walioshinda kesi na mifugo haijakabidhiwa, Waziri Ndumbao aliahidi kuwa watazifuatilia ili haki za walioshinda zisipotee.

Pia aliagiza wananchi waliolima katika hifadhi wapewe vibali maalum vya kuvuna mazao yao na baada ya mavuno wasirudi tena kwenye hifadhi.

Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi, akijibu hoja za wabunge kuhusu suala la ardhi kwenye hifadhi na ongezeko la watu alisema serikali imeshafanya uamuzi kwa kufuta mapori tengefu 12 yenye ukubwa ekari 707,659.4 ili yapangwe yaweze kutumika kwa shughuli za binadamu za kilimo na mifugo.




FURAHIA MAISHA
NA MAJI ASILIA

## HABARI KITAIFA

# Waziri aagiza wananchi wapewe elimu uzalendo

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mohamed Mchengerwa, ameutaka uongozi wa Chuo cha Utumishi wa Umma (TPSC) kutoa mafunzo yatakayoimarisha uzalendo na utaifa ili kuzalisha watumishi wa umma na Watanzania wazalendo watakaoshiriki vyema katika kujenga uchumi wa taifa.

Akizungumza katika mahafali ya 33 ya chuo hicho yaliyofanyika juzi katika Kituo cha Kimataifa cha Mikutano cha Julius Nyerere (JNICC) jijini Dar es Salaam, Mchengerwa alisema kutokana na kukosekana kwa uzalendo kwa baadhi ya Watanzania, ni muda mwafaka sasa kwa kila Mtanzania kuwa mzalendo kwa taifa lake kwa lengo la kulinda rasilimali za taifa, hivyo ni vyema chuo kikajikita pia katika mafunzo ya uzalendo na utaifa.

Mchengerwa alisema wahitimu wa chuo hicho wakiwa na uzalendo, watatumia vyema mafunzo waliyoyapata ili kuleta tija hususan katika kukuza uchumi wa taifa.

"Mafunzo mliyoyapata yasiishie hapa, bali yawe ni nyenzo na mkawe mabalozi wazuri kwa kutekeleza majukumu yenu kwa weledi mkubwa na uadilifu," Mchengerwa aliagiza.

Katika kuwajengea uwezo watumishi wa umma, Mchengerwa alitoa rai kwa viongozi wa taasisi za umma na halmashauri mbalimbali nchini kutenga bajeti itakayowawezesha watumishi wao kushiriki mafunzo katika chuo hicho yatakayowajenga kiutendaji.

Waziri huyo alisema kuwajengea uwezo watumishi wa umma ni mojawapo ya utekelezaji wa Ilani cha Chama Cha Mapinduzi (CCM)ya 2020/25, hivyo akaiagiza Bodi ya Ushauri na Uongozi wa chuo hicho kufanya mawasiliano kwa lengo la kuzihimiza wizara na taasisi zote za serikali ili watumishi wanaostahili kupata mafunzo katika chuo hicho wapate fursa hiyo.

Mchengerwa aliupongeza uongozi wa chuo na wakufunzi kwa kutekeleza majukumu yao ya msingi ya chuo na kuaigiza bodi na uongozi kutekeleza maelekezo ya viongozi mbalimbali ya kusogeza huduma kwa wananchi kwa kuanzisha matawi mengi zaidi ya chuo na kubuni mikakati mbalimbali itakayosaidia chuo kuwa cha mfano ndani na nje ya nchi.

Mwenyekiti wa Bodi ya Ushauri ya chuo hicho, Dk. Florence Turuka, alisema wahitimu wamepata mafunzo mazuri yenye weledi mkubwa na kuwasihi kutumia ujuzi na maarifa waliyoyapata kwa maslahi mapana ya taifa.

Mkuu wa chuo hicho, Dk. Selemani Shindika, alisema chuo hicho kilianzishwa mwaka 2000 chini ya Sheria ya Wakala Na. 30 ya Mwaka 1997 kupitia Mpango wa Uboreshaji Utumishi wa Umma (PSRP) kwa lengo la kubadilisha na kuboresha utumishi wa umma na kutoa mafunzo kuhusu utumishi wa umma, kuratibu na kujenga utamaduni mpya wa watumishi.

Dk. Shindika alisisitiza umuhimu watumishi wanaoajiriwa kwa mara ya kwanza kushiriki mafunzo elekezi katika chuo hicho ili kuwawezesha watumishi hao kufanya kazi kwa weledi na ufanisi.

Jumla ya wahitimu 7136 wa kozi 12 zinazotolewa na chuo hicho walitunukiwa astashahada ya awali, astashahada, stashahada na shahada katika fani mbalimbali.

# Mpango: Mtihani huu ni kipimo sahihi kwa Jafo

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MAKAMU wa Rais, Dk. Philip Mpango, ametaja kipimo kitakachotumika kupima utendaji wa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Selemani Jafo kuwa ni mafanikio ya utekelezaji wa kampeni kabambe ya kitaifa ya usafi na usimamizi wa mazingira nchini.

Aidha, ametoa wito kwa vyuo na watafiti kufanya utafiti wa kubaini sababu ya bei kubwa ya nishati mbadala na kushauri nini kifanyike ili kupunguza gharama za bidhaa hiyo na kuondokana na matumizi makubwa ya kuni na mkaa.

Dk. Mpango aliyasema hayo jana katika kilele cha maadhimisho ya siku ya mazingira duniani na uzinduzi wa kampeni hiyo yaliyofanyika kitaifa jijini hapa.

Alisema, Waziri Jafo mwenyewe ndio ameanzisha kampeni hiyo na atapimwa kulingana na mafanikio yake.

"Katika hili Mheshimiwa Jafo unisikilize, ninakutaka usimamie utekelezaji wa kampeni hii siku kwa siku, nisingependa kuona mambo yale yale kama ilivyokuwa zamani, sasa lazima uhakikishe hii kampeni inafanikiwa sana, unisamehe nitasema haya maneno hapa, lakini lazima niyaseme, kampeni umeianzisha mwenyewe na utapimwa kwa mafanikio ya hiyo kampeni."

Alisisitiza serikali kuendelea kuwachukulia hatua wahalifu wote wa mazingira na kampeni hiyo itaongeza uwajibikaji katika usimamizi.

"Kupitia kampeni hii wananchi watahamasishwa kushiriki katika shughuli za kuhifadhi mazingira kwenye maeneo yao, kampeni hii itakuwa ya kudumu na itaambatana na utoaji wa tuzo na zawadi mbalimbali kwa watakaofanya vizuri, zitatolewa kila mwaka ifikapo Juni 5," alisema.

Kadhalika, alisema Tanzania inaweza kuondokana na matumizi ya kuni na mkaa kwa kutumia nishati mbadala ikiwamo mafuta ya taa, gesi, umeme, nishati ya jua.

Alitoa wito kwa wafanyabiashara hasa wa gesi ya kupikia kubuni mbinu za kuwasaidia wananchi wenye kipato cha chini ili wamudu gharama kubwa za nishati mbadala.

Aidha, alisema serikali na wadau binafsi hawana budi kutekeleza miradi ambayo inalenga kuongeza matumizi ya nishati mbadala ya kupikia ikiwamo gesi asilia.

Makamu wa Rais alisisitiza matumizi hayo yameendelea kuongezeka hata mijini kwenye vyanzo vingine vya nishati.

"Mathalani Mkoa wa Dar es Salaam pekee unatumia zaidi ya magunia 500,000 ya mkaa kwa mwaka mmoja sawa na tani 45,000 ambazo ni sawa na mita za ujazo 75,000 za miti," alisema.

Alitaka wananchi waelimishwe kuachana na mila potofu zinazoharibu miti na misitu huku akitoa mfano wa kabila ambalo mtu akichoma pori na moto kwenda mbali wanaamini mtu huyo ataishi miaka mingi na kutaka halmashauri zikasimamie na kudhibiti uharibu huo.

Dk. Mpango alisema atakagua kila Mkuu wa Mkoa na Katibu Tawala wake suala la upandaji miti kwenye mikoa yao na itunzwe na kukua.

Awali, Waziri Jafo, alisema nchi imeanzisha kampeni hiyo kwa lengo la kuhamasisha utunzaji na uhifadhi mazingira katika maeneo mbalimbali nchini.

Mwenyekiti wa Mabalozi wa Kampeni ya Utunzaji Mazingira, Shekhw wa Mkoa wa Dar es Salaam, Mussa Salum, alisema watatumia weledi wao kuifanya Tanzania kuwa kioo cha utunzaji mazingira duniani.

Mwenyekiti wa Kamati Maalumu ya Uratibu wa Kampeni ya Mazingira nchini, Seif Ali Seif, alisema mabadiliko ya mazingira yamesababisha vipindi vya mvua na kiangazi kushindwa kutabirika kama zamani.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge, Mazingira, Viwanda na Biashara, David Mwakiposa, alisema kamati inashauri serikali ikaangalia matumizi ya nishati ya mkaa, kwa sababu Dar es Salaam licha ya wakazi wake kutumia nishati ya umeme kwa asilimia 90, lakini matumizi ya mkaa yanazidi asilimia 70.

Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Anthony Mtaka, alisema Mkoa wa Dodoma utahakikisha utunzaji mazingira unakuwa kipaumbele kama ambavyo serikali imekuwa ikisisitiza.


**KUPOTEA KWA CHETI**



**CHACHA MATIKO** anatangaza kupotelewa na cheti cha T**AALUMA YA STASHAHADA** chenye namba za usajili E0506-0303 kilichotolewa na **CHUO CHA UALIMU-MARANGU** mwaka **2015**,yeyote atakayekiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi

Polisi taarifa **SIR/RB/547/2019**



Form 281d

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**BUSINESS REGISTRATIONS AND LICENSING AGENCY**

**Advertisement of Winding-up Petition**
**Pursuant to section 281 of the Companies Act 2002**

IN THE MATTER OF: **MINISO TANZANIA COMPANY LIMITED**

A Petition to wind up the above named Company, of:

Address: **MINISO TANZANIA COMPANY LIMITED, P.O BOX 288, ILALA DAR ES SALAAM. Email: wallace.li@miniso.com Mob: +255763365399**

Presented on: **20th JANUARY 2021**

by: (name and address of petitioner) **MINISO TANZANIA COMPANY LIMITED, P.O BOX 288, ILALA DAR ES SALAAM**

Claiming to be THE COMPANY

will be heard at: (Name of Court) **THE HIGH COURT OF TANZANIA (COMMERCIAL DIVISION) AT DAR ES SALAAM WINDING UP CAUSE NO. 4 OF 2021 - (Before Hon. B.K Phillip, J.)**

On (date): **15TH JUNE 2021**

At (time): **11:30 AM**

(or as soon thereafter as the petition can be heard)

Any person intending to appear on the hearing of the Petition (whether to support it or to oppose it) must give notice of his intention to do so to the petitioner or his / its Advocate in accordance with Rule 3.16 of the Companies (Insolvency Rules) 2003 by 16:00 hours on the business day before the date of the hearing given above.

The Petitioner's Advocate is:
**ESTHER PETER**
**KKB ATTORNEYS AT LAW - OYSTER PLAZA SECOND FLOOR,**
**P.O BOX 13989, DAR ES SALAAM.**
**MOB: 0745770045**
**Email: info@kkbattorneys.co.tz**

Dated **5th JUNE 2021**

MAKALA MAALUM

# Mtoto kuzaliwa utumbo uko nje

## •Mabingwa Muhimbili wataja kiini cha ugonjwa na hali ilivyo
## •Mwanza, Kilimanjaro, Dodoma, Tanga na Mbeya vinara

**Na Mary Geofrey**

GASTROSCHISIS ni jina la kitaalamu la ugonjwa wa mtoto kuzaliwa utumbo ukiwa nje.

Wataalamu wa tiba katika Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH) wanasema tatizo linalosababishwa na hali ya ukuta wa tumbo kuwa wazi wanaozaliwa nalo watoto.

Matabibu hao wanabainisha kuwa takwimu zinaonyesha kati ya watoto 2,000 wanaozaliwa duniani kote, mmoja ana tatizo hilo.

Daktari Bingwa wa Upasuaji wa Watoto wa MNH, Zaituni Bokhari, anasema tatizo hilo limeenea duniani kote na idadi ya wagonjwa inaongozeka kila mwaka.

Anasema katika nchi za magharibi, takwimu zinaonyesha kati ya watoto 2,000 wanaozaliwa, mmoja ana tatizo hilo na katika nchi zilizoendelea ni asilimia nne ya watoto wanaopoteza maisha.

Anasema katika nchi changa watoto kuanzia asilimia 75 hadi 100 wanapoteza maisha, wakati Tanzania asilimia 90 hadi 100 wanaozaliwa na hali hiyo wanapoteza maisha.

Kadhalika, takwimu zinaonyesha wagonjwa 20 hadi 30 kwa mwaka wanatibiwa kutoka maeneo mbalimbali nchini na wengi hufika hospitalini wakiwa katika hali mbaya.

**CHANZO CHA TATIZO**

Dk. Zaituni anasema hakuna sababu ya msingi ya watoto kuzaliwa na tatizo hilo isipokuwa kuwapo kasoro kadhaa.

Anasema moja ya kasoro ni mtoto kuzaliwa akiwa hajatimia miezi tisa, akifafanua kuwa anakuwa na uwezekano mkubwa wa kuwa na tatizo hilo kwa sababu viungo vyake vinakuwa havijakamilika.

Anasema mama mjamzito anapokuwa na magonjwa sugu kama moyo, figo, Ukimwi na sukari yanayomfanya atumie dawa kwa muda mrefu, ni rahisi kuzaa mtoto mwenye hitilafu hiyo.

Hata hivyo, daktari bingwa huyo anaweka wazi kuwa siyo wanawake wote wenye magonjwa hayo sugu wanazaa watoto wenye tatizo hilo hasa wakizingatia masharti ya watoa huduma wa afya wakati wote wa ujauzito.

"Mimi nina msemo wangu wa kuwaambia wanawake wajawazito waangalie nini wanakula, wafikirie kuhusu watoto wao," anasema.

Dk. Zaituni anasema mama mjamzito kuhudhuria kliniki zote kunaweza kuepuka kuzaa mtoto mwenye hitilafu hiyo kwa kuwa kutohudhuria kunasababisha kukosa kupatiwa kinga muhimu za mtoto akiwa tumboni.



Dk. Zainabu Bokhari.

**KWANINI WENGI HUFARIKI?**

Dk. Zaituni anasema nchini watoto waliozaliwa na tatizo hilo, iliaminika hawawezi kupona na hata watoa huduma za afya walikuwa wakiamini hivyo.

Anasema kutokana na kukithiri kwa tatizo hilo, madaktari waliamua kufanya utafiti wa kubaini sababu za vifo kuwa vichache katika nchi zilizoendelea.

Kwa mujibu wa mtaalamu huyo, utafiti ulibaini nchi zilizoendelea zina mfumo wa kubaini tatizo tangu mtoto akiwa tumboni kama ana hitilafu katika mwili wake au viungo vyake.

"Wameenda mbali zaidi hata kuanza kumtibu mtoto akiwa bado yupo ndani ya tumbo la mama yake wakati sisi bado hatujafikia hatua hiyo lakini ndiko tunakokwenda," anasema.

Dk. Zaituni anasema utafiti pia ulibaini nchi zilizoendelea zina vifaa vya kutatua tatizo hilo.

Anasema mtoto anapozaliwa na tatizo hilo, anatakiwa kufunikwa utumbo wake kwa kutumia teknolojia maalum (silo bags) iliyotengenezwa na vifaa maalum.

"Kwanza tulibaini watoto hawa wanapozaliwa katika nchi hizo wanakuwa katika mazingira mazuri ya kuwahi kupata matibabu na wanapelekwa kwenye huduma nzuri zaidi," anasema.

Dk. Zaituni anasema pia walibaini watoa huduma wa nchi zilizoendelea wana elimu ya kutosha ya namna ya kumhudumia mtoto mwenye tatizo hilo.

"Nchini kwetu elimu inahitajika zaidi kwa sababu ya mazingira wanakozaliwa watoto hawa kutoka maeneo ya pembezoni ambako hutumia muda mrefu hadi kufika Muhimbili," anasema.

Daktari bingwa huyo anasema katika zahanati, vituo vya afya na hosptali za mikoa ndiko wanakozaliwa watoto hao na hadi kufikishwa Muhimbili wanakuwa katika hatua mbaya.

Anasisitiza elimu inahitajika katika hospitali hizo ili watoa huduma wanapopata mtoto wa aina hiyo wajue nini cha kufanya.

Abainisha kuwa watoto wanaozaliwa na tatizo hilo husumbuliwa na tatizo la upumuaji, hivyo hutakiwa kuwekwa kwenye mashine ya upumuaji na pia hulishwa chakula kwa njia ya mshipa kwa sababu hawawezi kunyonya wala kula chochote.

Dk. Zaituni anasema walifanya utafiti na nchi nyingine za Afrika ambazo ni Malawi, Zambia na Ghana ili kuangalia kwa nini watoto wanaozaliwa utumbo ukiwa nje wanakufariki dunia, wakabaini sababu hizo.

Anasema waliomba kufanya mafunzo na madaktari bingwa wa hospitali kutoka nchi zilizoendelea kwa muda wa miaka miwili.

Dk. Zaituni anasema walikubaliwa kufanya utafiti huo kwa kukubaliana kila nchi kuanza kuwahudumia watoto wenye matatizo hayo kulingana na vifaa na namna wanavyoweza kuwapa huduma ili kuona njia ya kusaidia kuwaokoa.

"Kwa Tanzania tulitumia zana za matibabu za ndani ya nchi, tulikuwa tukipokea watoto kutoka Tanga, Mtwara, Morogo na walikifika wakiwa wameshapata maambukizi ya bakteria," anabainisha.

Anafafanua zaidi kuwa watoto hao walikuwa wanapokewa wakiwa wameshapigwa baridi kali kwa sababu wanazaliwa na kusafirishwa.

"Ilikuwa ni changamoto kubwa sana kwa sababu vifaa tulivyokuwa tukitumia hapa Muhimbili, watoto wote waliokuwa wanazaliwa na tatizo lazima wanapelekwa chumba cha upasuaji ili kuhudumiwa na daktari bingwa wa watoto," anasema.

Anabainisha kuwa walikuwa wanatumia mpira wa mkojo wanaowekea wagonjwa ambao uliundwa na kuwa kama begi maalum la kuhifadhia utumbo wa mtoto uliotoka nje.

Anasema kwa sababu vifaa vilikuwa vya kienyeji, mipira ilikuwa inapasuka na utumbo kutoboka na hivyo mtoto kupoteza maisha.

Dakatri bingwa huyo anasema mtoto pia alikuwa akichomwa sindano za usingizi ambazo zilikuwa na madhara kwake kwa sababu bado ni mchanga, hivyo kupoteza maisha.

Kadhalika, alisema kikwazo kingine ni mtoto anapopokewa usiku anakosa daktari bingwa wa kumtibu, hivyo kutumia zaidi ya saa nne kufuatwa nyumbani na kusababisha mtoto kucheleweshewa huduma.

**MATIBABU YAKE**

Dk. Zaituni anasema baada ya kubaini vikwazo hivyo, kwanza walipatiwa msaada wa mabegi maalum ya kuhifadhia utumbo huo badala ya kutumia mipira.

Anasema pia walianza kutoa elimu kwa watoa huduma wote wa hospitali zote za Mkoa wa Dar es Salaam na wilaya chache za Mkoa wa Pwani ili wanapopata mgonjwa wa aina hiyo, waanze kumpatia huduma sahihi badala ya kumsubiri daktari bingwa.

Anasema baada ya kuchukua hatua hizo, walifanya utafiti mwingine wa kuangalia wanavyotoa huduma bila kumpeleka mtoto chumba cha upasuaji wanapata matokeo gani.

Dk. Zaituni anasema hospitali nyingi sasa zinatoa huduma ya kwanza ya kumtafutia plastiki safi ya kuhifadhi utumbo huo kabla ya kumpeleka Muhimbili.

Anasema awali watoto waliokuwa wanapatikana walikuwa wanajazwa kitambaa cheupe maalum (gozi) kilichojazwa maji maji wakiamini zitasaidia kuhifadhi utumbo huo ili usiwe mkavu.

Anasema njia hiyo ilikuwa ikiujaza utumbo maji na kusababisha joto la mwili la mtoto kupungua na kupata maambukizi ya bakteria.

Dk. Zaituni anasema walitengeneza mabegi hayo maalum ya kuhifadhia utumbo wakayasambaza katika hospitali za wilaya za Mkoa wa Dar es Salaam ili kutoa huduma ya kwanza kwa watoto hao.

"Baada ya kumaliza utafiti huo wa mwaka mmoja, tulisadia kuokoa maisha ya watoto kwa asilimia 78 kutoka asilimia 90 hadi 100 waliokuwa wakipoteza maisha," anabainisha.

Anasema baada ya utafiti huo, walipanga kuanza kutoa elimu nchi nzima kwa kuanza na mikoa ya Mwanza, Kilimanjaro, Dodoma, Tanga na Mbeya.

Dk. Zaituni anasema waliamua kuanza na mikoa hiyo kwa sababu inaongoza kwa kuwa na watoto wengi wenye tatizo hilo.

"Tuliamua kuanza kutafuta wadhamini ambao wamepatikana watakaofadhili mikoa miwili ya Mwanza na Dodoma, katika kampeni ya 'Okoa Maisha ya Watoto Wanaozaliwa Utumbo Nje'," Dk. Zaituni anahitimisha.

HABARI KITAIFA

# SUA kunoa ujasiriamali

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

CHUO Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) kwa kushirikiana na Shirika la Kusaidia Sekta Binafsi ya Kilimo ( Wakfu wa PASS), wameanzisha Kituo Atamizi cha Vijana kinachoendesha mradi wa kulea na kufundisha vijana ujasiriamali kwenye sekta ya kilimo biashara.

Tayari kituo hicho kina vijana 92 ambao ni wahitimu wa vyuo vikuu, vyuo vya kati na shule za msingi waliojiunga Oktoba na Novemba mwaka jana wakishiriki mafunzo kwa kipindi cha mwaka mmoja.

Makamu Mkuu wa SUA, Profesa Raphael Chibunda, alisema hayo mbele ya Mkuu wa Chuo Kikuu hicho, Jaji mstaafu Joseph Warioba wakati wa mahafali ya 37 ya chuo hicho yaliyofanyika juzi Kampasi ya Edward Moringe Sokoine mjini Morogoro.

Katika mahafali hayo, jumla ya wahitimu 149 (wanaume 92) walitunukiwa vyeti vya kuhitimu masomo yao kwenye ngazi ya astashahada, stashahada, shahada ya kwanza, shahada ya umahiri na shahada ya uzamivu iliyokuwa na wahitimu 15.

Profesa Chibunda alisema miundombinu iliyojengwa kwenye Kituo Atamizi ni pamoja na vitalu nyumba 87 na maeneo ya mashamba kwa ajili ya kilimo cha nje na miundombinu ya maji kwa ajili ya umwagiliaji.

"Madhumini ya kituo hiki kwa ajili ya kuzalisha mazao kibiashara chini ya uangalizi maalum na kuwafundisha vijana wanaohitimu kutoka vyuo vya elimu ya juu, kati na shule za msingi nchini," alisema.

Profesa Chibunda alisema vijana hao wanapohitimu kutoka kwenye kituo hichop watakwenda kubadilisha sura ya kilimo cha nchi ili kuwe na tija zaidi katika kuchochea ukuaji wa uchumi.

Katika hatua nyingine, kiongozi huyo wa chuo alisema kwa kipindi cha Januari mwaka huu hadi sasa, chuo kimepata miradi mipya minane ya utafiti yenye thamani ya Sh. bilioni 2.2 na imefadhiliwa na wadau mbalimbali kutoka ndani na nje ya nchi.

Alisema chuo kinaendelea kutekeleza mikataba ya ushirikiano kwenye maeneo ya taaluma, utafiti, ugani na miradi ya maendeleo na taasisi nyingine za ndani na nje ya nchi zaidi ya 90.

Mwenyekiti wa Baraza la Chuo, Jaji Mkuu mstaafu, Mohamed Chande, alisema utekelezaji wa Mpango Mkakati wa Chuo wa Awamu ya Nne 2016-2021 ulioanza kutekelezwa Julai Mosi, 2016, umetekelezwa kwa asilimia 74.45 na kutumika Sh. milioni 39.95.

Alisema kwa niaba ya Baraza la Chuo hicho, anaishukuru serikali kwa ruzuku na fedha za maendeleo inayotoa kwa chuo kwa kuwa ni dhahiri bila fedha hizo kisingeweza kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

Alitumia fursa hiyo kuwaasa wahitimu wa chuo hicho kutumia elimu waliyoipata katika kujenga taifa na wawe wenye nidhamu na uadilifu katika kazi zao za kila siku.

# Serikali yazuia wananchi kuuziwa nguzo za umeme

**Na Romana Mallya**

WAZIRI wa Nishati, Dk. Medard Kalemani, amepiga marufuku wananchi kuuziwa nguzo za umeme na amesisitiza bei ya kuunganisha huduma hiyo ni Sh. 27,000 iwe Shirika la Umeme (TANESCO) au Wakala wa Nishati Vijijini (REA).

Dk. Kalemani aliyasema hayo juzi bungeni jijini Dodoma wakati wa majumuisho ya kupitisha makadirio ya mapato na matumizi ya wizara hiyo kwa mwaka ujao wa fedha.

Alisema iwe TANESCO au REA bei ya kuunganishwa umeme ni Sh. 27,000 kwa mjini na vijijini.

"Bei ya kupeleka umeme ukiondoa jijini Dar es Salaam ambako hawahitaji kwa sasa, tayari wanao, maeneo yote nchini ni Sh. 27,000, niwaelekeze TANESCO atayesuasua kutekeleza agizo hili hajitaki na atakuwa hana kazi, hayo ndiyo maelekezo ya serikali," alionya.

Kuhusu wananchi kuuziwa nguzo, Waziri Kalemani alisema serikali imezigharamia kwa asilimia 100 na kwamba zipo na mahitaji yake kwa mwaka ni milioni 2.8 na zilizopo ni milioni 4.9.

"Makandarasi, mameneja wa TANESCO msijiingize kwenye mtego wa kusema mwananchi ananunue nguzo, tutakushughulikia mapema usiku na mchana, jipangeni.

"Haiwezekani wananchi wote waishi ndani ya mita 30 kutoka kwenye nguzo, muwe wabunifu, fanyeni kazi kwa kasi na weledi," aliagiza.

Waziri huyo alisema lipo tatizo la ucheleweshaji wa wananchi kuunganishiwa umeme na kueleza kuwa zipo hatua wameanza kuchukua ambazo ni za kuwapima mameneja ili apande cheo, vigezo ni viwili kuunganisha umeme kwa wateja kwa kasi na huduma wanayoitoa kwa wananchi. Waziri huyo pia alitoa miezi miwili kwa mameneja wanaodaiwa na wateja ambao wamelipa fedha zao ili waunganishiwe umeme na hawajafanya hivyo, wakamilishe vinginevyo hatua za kisheria dhidi yao zitachukuliwa.

Kuhusu kukatika kwa umeme, Waziri Kalemani alisema zipo sababu mbalimbali ikiwamo nguzo kuchakaa, wakati mwingine kuchomwa moto au kugongwa na nyaya kukatikana.

Alisema wametenga bajeti ya Sh. bilioni 85.8 ili kurekebisha dosari kama hizo na kwamba vijiji vilivyobaki ambavyo havijaunganishiwa umeme, wamepeleka makandarasi na wiki ijayo watapatikana ili mikoa yote wawe wamefika maeneo ya kazi.

Pia alisisitiza kuwa mradi wa umeme vijijini haubagui nyumba na ule wa vitongoji wametenga Sh. bilioni 366 kwa ajili ya kupelekea nishati kwenye vitongoji vyote.

"Yapo maeneo ambayo siyo vijiji yanaitwa mitaa lakini ukitazama siyo mitaa hasa maeneo ya majiji, manispaa, halmashauri za miji yapo mengi tumeanza kushughulika nayo tumebaini maeneo 637 yakiwamo Dar es Saalam, tumetenga Sh. bilioni 160," alisema.

Waziri Kalemani alisema kuanzia wiki ijayo wizara itatoa mafunzo kwa wabunge ambao maeneo yao kuna miradi inayotekelezwa ili kuwajengea uwezo na ufahamu namna ya wananchi wao kushiriki miradi hiyo ya kimkakati

# Jafo asisitiza takwimu Bonde la Wami Ruvu

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Selemani Jafo, amesema takwimu zinazotolewa na Bodi ya Maji Bonde la Wami Ruvu ni muhimu kwa kuwa zimekuwa zikiisaidia serikali hususani wizara yake kuchukua tahadhari kuhusu mabadiliko ya tabianchi kwenye vyanzo vya maji ikiwamo mito na mabwawa.

Waziri Jafo alitoa kauli hiyo jana jijini Dodoma wakati wa maadhimisho ya Wiki ya Mazingira alipotembelea Banda la Maonyesho la Bodi ya Maji Bonde la Wami Ruvu.

Alisema rasilimali maji ni muhimu kwa maendeleo na ustawi wa binadamu, hivyo akaitaka bodi hiyo kuwa mstari wa mbele kuiongoza serikali kupitia takwimu zake katika kuchukua hatua stahiki za kukabiliana na athari za mazingira kwenye vyanzo vya maji.

"Ofisi yenu ni muhimu sana, lakini inatusaidia vilevile kutoa tahadhari watu wasivamie vyanzo vya maji kwa sababu wakivamia mambo yote yanakuja kuharibika.

"Kwa mfano leo hii tunajenga lile Bwana la Nyerere, kama watu watavamia vyanzo vya maji, lile bwana litakuwa halijai," alisema.

Wiki ya Mazingira Duniani inafikia kilele chake leo, serikali inatarajia kuzindua Kampeni Kabambe ya Kuhamasisha Jamii Kutunza na Kulinda Mazingira.




Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Udhibiti matukio ya ujangili utapaisha utalii

**MATUKIO** ya ujangili wa wanyama nchini yamekuwa tishio na kuathiri sekta ya utalii kwa kiasi kikubwa katika miaka ya nyuma. Ujangili wa wanyama unasababisha wanyama hao ambao ndio kivutio kikubwa cha utalii kupungua na wengine kuhama kukimbilia nchi za jirani.

Tanzania inategemea sekta ya utalii kwa kuiingizia fedha za kigeni na kwa mwaka 2018, jumla ya Sh. trilioni sita zilitokana na mapato ya fedha za kigeni.

Sekta hiyo inapopata hasara ya kupoteza vivutio vyake, nchi pia inaathirika kwa kupungua kwa mapato ya fedha za kigeni kwa sababu ya kukosa watalii wanaokuja kuona vivutio hivyo.

Juzi serikali ilitangaza habari njema za kupunguza matukio ya ujangili kwa asilimia 90 na kuzuia matukio 302 kabla hayajatendeka.

Taarifa hizo njema zilitangazwa na Waziri wa Maliasili na Utalii, Dk. Damas Ndumbaro, jijini Dodoma alipokuwa akiwasilisha makadirio na mapato ya wizara hiyo.

Wizara hiyo pia inaendelea kuimarisha ulinzi wa rasilimali za maliasili na kudhibiti ujangili, biashara haramu ya nyara, uvunaji haramu wa mazao ya misitu na uvamizi wa maeneo yaliyohifadhiwa kwa kushughuli za kilimo, ufugaji na makazi.

Udhibiti wa ujangili umesaidia kwa kiasi kikubwa kurudisha idadi ya wanyama aina ya tembo ambao walikuwa hatarini kutoweka kutokana na majangili hao kuwawinda ili kupata meno yao na kwenda kuyauza ughaibuni.

Wanyama wengine ambao pia walikuwa katika hatari ya kupungua ni faru, lakini kutokana na udhibiti tunaambiwa idadi yao imeanza kuongezeka.

Wizara ya Maliasili na Utalii pia inajivunia na wageni wanaoendelea kuingia nchini kwa kuja kuangalia wanyama kwenye hifadhi za taifa na maeneo mengine yenye vivutio vya asili.

Imeelezwa kuwa watalii wa nje 437,000 hadi 620,867 waliingia nchini licha ya kuwapo kwa tishio la janga la corona.

Wizara hiyo kwa mwaka jana ilitarajia kupokea jumla ya watalii 1,867,000, makisio hayo ni kabla ya kuingia kwa janga la corona nchini.

Hata hivyo, Tanzania imefanikiwa kuwa miongoni mwa nchi chache za Afrika zilizopata muhuri wa Safe Travel wa Baraza la Usafiri na Utalii Duniani (WTTC) kwa kigezo cha hatua za kukabiliana na maambukizi ya corona.

Kwa mujibu wa Waziri wa Maliasili na Utalii, muhuri huo hutolewa kwa kuzingatia nchi husika kutoa mwongozo wa kiafya wa kuzingatiwa na wasafiri wanaoingia na kutoka nchini.

Tanzania pia imeendelea kufungua masoko mapya ya utalii ikiwamo Urusi, Poland na Ukraine na kuorodheshwa na nchi ya Urusi kuwa miongoni mwa nchi tatu duniani ambazo ni salama kwa wananchi wake kutembelea.

Hatua hii ya wageni kuendelea kuitembelea Tanzania inaihakikishia nchi kujiingizia mapato ya kigeni hasa ikizingatiwa kuwa sekta ya utalii ndio kinara kwa mapato ya fedha za kigeni.

Ni matumaini yetu kuwa mikakati ya kudhibiti ujangili itaendelea kuimarishwa na Tanzania kuendelea kung'ara katika sekta ya utalii.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Usafi wa mazingira usisubiri maadhimisho

Na Sabato Kasika

**MAZINGIRA** yanatafsiriwa kuwa ni jumla ya mambo yote yanayomzunguka kiumbe katika maisha yake, na kwamba yanaundwa na vitu mbalimbali vikiwamo vya asili kama vile misitu, milima, maziwa, mabonde, mito na bahari.

Pamoja na hayo, mazingira mengine yanaweza kuwa ya kutengenezwa na binadamu kuanzia majengo, viwanda na viti vingine vingi, lakini pia kile ambacho anakiona ni mazingira yake.

Wataalam wa mazingira wamekuwa wakishauri watu kuwa makini katika suala la utunzaji wa mazingira yao, kwa kuwa wanaweza kusababisha uharibifu kama vile uchafuzi wa hewa, wa bahari, ardhi na maeneo mengine.

Vilevile kilimo, ufugaji na mvua, navyo uathiriwa na uchafuzi wa mazingira, hivyo mkazo unawekwa katika utunzaji wa mazingira kwa kupanda miti kwa wingi, kutunza vyanzo vya maji.

Katika maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani, ambayo yalifikia kilele chake jana, jamii inakumbushwa kuwa suala la uhifadhi, utunzaji, usimamaizi na usafi wa mazingira lisisubiri kufanyika wakati wa maadhimisho pekee.

Lakini pia, watumishi wa umma, wadau wa mazingira na vyombo vya habari kwa pamoja wanatakiwa kushiriki kikamilifu katika kuimarisha uhifadhi na utunzaji wa mazingira wakati wote.

Ni wakati wa kutoa tamko la serikali kuhusu maadhimisho ya mwaka huu, Waziri Mkuu Kassim Majaliwa anahimiza hayo na kusema, serikali itaendelea kulinda na kuhifadhi mazingira kwa kushirikiana na wadau mbalimbali.

Mbali na hilo, anasema, nguvu kubwa itaelekezwa katika matumizi ya nishati mbadala ili kuepuka athari za mazingira, kwa kuwa takwimu zinaonyesha kuna matumizi makubwa ya kuni na mkaa kutokana na ongezeko kubwa la watu.

Kilichoelekezwa na Waziri Mkuu ni cha muhimu kwa jamii na taifa kwa ujumla, lakini pia kuna haja ya kujielekeza na huku ambako wapo baadhi ya watu wanaoendelea kuharibu na kuchafua mazingira.

Suala la nishati mbadala haliepukiki, lakini pamoja na mkakati huo wa serikali wa kujielekeza katika matumizi ya nishati mbadala ili kulinda mazingira, wafanyabiashara wadogo, abiria na waenda kwa miguu nao waguswe.

Imekuwa ni jambo la kawaida kukuta mfanyabiashara anapanga mbao juu ya mtaro wa maji ya mvua kisha anaweka bidhaa zake, huku taka anazozalisha akitupa ndani ya mtaro kana kwamba ndiyo sehemu ya kuhifadhia taka.

Baadhi ya abiria nao wakati mwingine wanaweza kuwa katika daladala wanakula vyakula kama mahindi, wanapomaliza, wanafungua dirisha na kutupa magunzi nje bila kujali kwamba wanachafua mazingira.

Mtindo huo pia uko kwa wale wananunua maji, wanapomaliza kunywa, hutupa chupa nje wafanyavyo wanaonunua vitu mbalimbali na kuvitumia wakiwa ndani ya vyombo vya usafiri.

Si hao tu, bali hata wale wanaofanya biashara ya kuuza chakula, baadhi yao husafisha vyombo na kumwaaga maji kwenye mitaro, huku yakiwamo mabaki ya vyakula kana kwamba ndiyo eneo na kutunzia taka.

Kwa ujumla ni kwamba huo nao ni uharibifu na uchafuzi wa mazingira, ambao ni vyema ukatafutiwa njia za kuumaliza ili wahusika waendelee na shughuli zao bila kusababisha kero kama hiyo.

Ninaamini kwamba hilo litawezekana iwapo kile alichosema Waziri Mkuu kitatekelezwa, ambacho ni jamii usimamizi na usafi wa mazingira kutosubiri kufanyika wakati wa maadhimisho pekee.

Maadhimisho hufanyika Juni 5, kila mwaka na Tanzania huungana na nchi nyingine duniani kuiadhimisha, lakini kwa mwaka huu hakukuwa na maadhimisho ya kitaifa, badala yake kila mkoa umeadhimisha kivyake.

Lengo la maadhimisho ya mazingira huwa ni kuhamasisha jamii kuelewa masuala yahusuyo mazingira na kuwa mstari wa mbele katika kuchukua hatua za kuhifadhi na kulinda mazingira.

Huwa pia ni fursa kwa jamii kufahamu kwamba ina wajibu wa kuzuia madhara na mabadiliko hasi katika mazingira na kuhamasisha kufanya mazingira yao kuwa salama na masafi katika maisha yao.

Binafsi ninaamini kuwa kila mmoja wetu akitunza mazingira kwenye eneo lake itakuwa rahisi kuepuka uchafuzi na uharibifu huo, ambao unatajwa kuwa una athari nyingi zikiwamo za kiafya.

SAFU

## KWA MASLAHI YA TAIFA

# Haki sio hisani, ni stahiki



Na Pascal Mayalla

**Waandishi wa habari wenye uwezo wa kuandika habari za uchunguzi, wanafanya kazi kama polisi. Mimi pia niko kwenye kundi hilo, na lengo la makala hizi sio kukosoa, bali kuonyesha upungufu ambao DPP mpya anatakiwa kuufanyia kazi.**

WIKI iliyopita, niliishia kwenye hoja ya "haki iliyocheleweshwa ni haki iliyo kiukwa" (justice delayed is justice denied), leo naendelea na makala hii, bado nikiangazia ofisi ya DPP ili kumsaidia DPP mpya maeneo ya kuangazia.

Mfumo rasmi wa utoaji haki unaposhindwa

Ingawa sijakutana rasmi na mtuhumiwa yeyote, kabla ya kuandika makala hii, kwa sababu hakuna ambaye angekubali iandikwe kwa uoga wa kesi iliyo mahakamani hairuhusiwi kujadiliwa, ukweli ni kuwa, kinachokatazwa na kujadili mwenendo wa kesi ambao unaweza kuingilia uhuru wa mahakama, lakini kutaja kuna kesi ambayo uchunguzi unaendelea kwa zaidi ya mwaka wa nne sasa na bado haijasikilizwa, sio kuingilia uhuru wa mahakama, bali ni kuangazia eneo muhimu la uchunguzi lenye udhaifu mkubwa.

Waandishi wa habari wenye uwezo wa kuandika habari za uchunguzi, wanafanya kazi kama polisi. Mimi pia niko kwenye kundi hilo, na lengo la makala hizi sio kukosoa, bali kuonyesha upungufu ambao DPP mpya anatakiwa kuufanyia kazi.

Watu wote wanaoteseka katika magereza ya Tanzania miaka na miaka kwa kukosa haki, kwa sababu ya kitu kinachoitwa uchunguzi unaendelea. Kesi zingine usikilizwaji bado hata haujaanza kwa zaidi ya miaka minne sasa, huu ni uchunguzi gani? Udhaifu wa uwezo wa vyombo vyetu kufanya uchunguzi, usisababishe watuhumiwa kupoteza haki zao, ukisha kaa jela miaka mitano, ukakutwa huna hatia, hakuna kiwango chochote cha fidia kinaweza kuufidia muda uliopotea isipokuwa ni Mungu tu!.

Watuhumiwa wanastahili kutendewa haki, na kwa waumini wa kitu kinachoitwa 'karma' ambacho mimi, ni muumini, naamini inawezekana kabisa ni karma ya ukosefu wa haki inayotokea Tanzania, inaweza kuchangia kuondoka mapema kwa baadhi ya wapendwa wetu, ambao tunawapenda sana, lakini Mungu akaamua kuingilia kati na kwa kuwapenda zaidi na saa hizi wako naye peponi.

Usawa uko wapi Mbele ya Sheria?

Kifungu cha 7 cha Azimio la Kimataifa la Haki za Binadamu (UDHR) kinasema: "Watu wote ni sawa mbele ya sheria na wana haki sawa bila ubaguzi wowote mbele ya sheria." Kila mtu lazima atendewe haki sawa sawa mbele ya sheria bila kujali rangi, jinsia, kabila, dini, ulemavu, au sifa zingine, bila upendeleo au ubaguzi. Tanzania imeliridhia Azimio hilo na kuliingiza ndani ya Katiba yetu, hivyo utoaji wa haki ni takwa la kikatiba, uvunjwaji wowote wa haki za binadamu ni ukiukwaji wa Katiba.

Unapowashitaki watu kwa kosa la jinai la uhujumu uchumi inamaanisha fedha hiyo inayotakatishwa ni fedha chafu, fedha ya wizi, ni ama zimeibwa, ama zimepatikana kwa njia isiyo halali.

Lakini kesi iliyofunguliwa ya jinai, ya utakatishaji fedha, halafu wakati huo huo, kufungua kesi nyingine ya madai kudai pesa ile ile, ni kinyume cha sheria ya double jeopardy, hii inamaanisha kudai pesa chafu iliyoibiwa, katika kesi moja ya jinai, halafu ifunguliwe kesi nyingine, ya madai na kutafuta suluhu ya amani. Kitendo cha kuigeuza pesa iliyopatikana kwa jinai ya uhalifu, na kuja kudai fedha hizo hizo kwenye kesi ya madai, ni sawa na utakatishaji wa fedha.

Kwa maoni yangu, sio haki kwa DPP kuwafungulia watuhumiwa kesi ya jinai ya uhujumu wa uchumi na utakatishaji fedha, halafu hapo hapo, wakafungua kesi nyingine ya madai, kwa DPP huyo huyo kuzidai tena fedha hizo.

**Kwa maoni: +255 754 270403**

**Watuhumiwa wanastahili kutendewa haki, na kwa waumini wa kitu kinachoitwa 'karma' ambacho mimi, ni muumini, naamini inawezekana kabisa ni karma ya ukosefu wa haki inayotokea Tanzania, inaweza kuchangia kuondoka mapema kwa baadhi ya wapendwa wetu...**

## MADONGO YA MGAGAGIGIKOKO

# Tanzania ya wanadamu na wanamaji



Na Joseph Kulangwa

**Lakini humo humo, kuna waliokuwa hawasemi wakati huo kwa sababu ya nidhamu ya uoga na kuna wanaosema sasa kwa sababu ya unafiki tu. Walizoea kuimba mapambio ili wapate hulua na sasa wanayaendeleza lakini hulua hakuna.**

NASIKIA na nimekuwa nikisikia kwa watu mbalimbali wakisema eti tabasamu limerejea miongoni mwa Watanzania. Wengine hawasemi tabasamu wanasema furaha imerejea kwa Watanzania.

Utajiuliza ilikwenda wapi? Ilikuwa wapi? Likizo? Inawezekana, kwa sababu lisemwalo lipo kama halipo linakuja! Ukiwasikiliza sana, utajikuta unakuja na ile methali ya wahenga, kwamba paka akiondoka panya hutawala!

Ukisikiliza ya vijiweni na hata katika baadhi ya mikutano rasmi na isiyo rasmi, utasikia kauli ambazo kuna nyakati hususan katika miaka mitano na ushei iliyopita, usingezisikia.

Wengine utasikia wanashangaana na kuulizana, hivi wewe wakati uke ungeweza kuyasema haya? Unajiuliza hivi kwa nini asingeweza kuyasema haya? Ndipo unapopata jibu, kwamba kulikuwa na tatizo la kusema.

Watanzania ni watu rahim sana, ukitaka wasiseme kwa kweli hawatasema, lakini ukitaka waseme watasema tu tena kwa sauti kubwa. Wakati ule kwa kweli kama ulithubutu kusema kile kilichoonekana ni kibaya kwa baadhi ya watu mh! Cha moto ungekiona.

Leo unaweza kusema tu ilimradi usitukane, sema ukosoe lakini kwa lugha ya staha. Mwenzio akikosea ukamsema kwa staha ataelewa na atajisahihisha, lakini ukimtukana, ah utakuwa unatafuta lako jambo.

Lakini humo humo, kuna waliokuwa hawasemi wakati huo kwa sababu ya nidhamu ya uoga na kuna wanaosema sasa kwa sababu ya unafiki tu. Walizoea kuimba mapambio ili wapate hulua na sasa wanayaendeleza lakini hulua hakuna.

Mimi Rais Samia binti Suluhu Hassan alinifurahisha siku aliyosema kuwa atateua watu bila kuangalia itikadi, dini, sura wala rangi, na juzi akasema tena kuwa anateua hata wapinzani kwa sababu ni Watanzania.

Hapo anagusa nyoyo za watu kwa hisia tofauti, kuna wanapofurahi lakini kuna wanaochukia. Wanaofurahi ni kama wale wanaoamini kama yeye kuwa vyama visitugawe, lakini wanaokasirika ni wale wasemao ukimchagua mpinzani hakuna maendeleo.

Enzi zile ukisikia kuwa ah mradi huu wa bandari ya naniliu haufai kabisa, hawa macho madogo wanataka kutuibia na kutudhulumu tu kiuchumi. Wale wale waliosema hivyo, leo wanasema hakuna mradi bomba kama huo.

Ukisikia enzi hizo, kwamba sheria hii ya mifugo iingiayo hifadhini ikakamatwa, na kutaifishwa ni nzuri na itakomesha tabia mbaya ya wafugaji, leo utasikia ah hivi nani aliitunga hiyo? Tulilala au tulisafiri?

Ukiwaona enzi hizo wakipinga kuwapo Uviko-19 na kuhubiri kutupa kule barakoa na kutamba kuwa kilichopo ni changamoto za kamasi tu, leo wanajifunika gubigubi mibarakoa mpaka sura zinawababilika!

Wakibugia mchanganyiko wa tangawizi, pilipili kichaa, vitunguu saumu, na kujifukiza majani ya miti wakitangaza operesheni nyungu awamu tofautitofauti, leo si wale mabanda ya nyungu katika hospitali kubwa yanataka kugeziwa vibanda vya mawakala wa simu!

Watanzania ukiwafuata utaumbukia shimoni bila kujua. Uwe makini sana kuwasikiliza kwa sababu ni bendera fuata upepo, ni vinyonga kama huwajui, wakiwa hapa wanabadilika rangi, wakiwa CCM utawaona ni wa kijani-njano, wakiwa Chadema wanakuwa nyekundu-nyeupe-bluu!

Ndiyo sababu unawaona kila siku wanahama vyama, watotako wanakusema vibaya, waendako wanakusema vizuri, lakini warudiko wanakusema vizuri waondokako wanakusema vibaya. Hao ndio Watanzania aka Wabongo.

Paka akiwapo, kila panya anaimba kumpongeza, lakini aondokapo tu, panya wanamtukana wakirukaruka kwenye kitanda chake, na kutafunatafuna kila wakikutacho kwa furaha yao.

Leo hii ukiacha wachache wanaogugumia maumivu ya kuondokewa, nani anakumbuka kuwa tulikuwa na kiongozi akafanya haya na yale akaondoka? Ndio kwanza wanafanya yao na kufuta yale.

Ni kazi sana binadamu kubaki na msimamo ulionyooka katika maisha yake, ndiyo sababu tuna binadamu, tuna binamaji; binadamu ni mwenye msimamo usiotetereka, anayesimamia ukweli, binamaji ni anayeyumba kimsimamo. Leo akisema ah! Kesho atasema eh! Mwogope sana.

**Alamsiki!**

SAFU

## KONA YA UKWELI

# Itafutwe njia kukabili wahamiaji haramu



Na Thobias Mwanakatwe

**Kwa kiasi kikubwa wanaowasafirisha wahamiaji hawa wanatajwa kushirikiana na Watanzania wasiokuwa waaminifu, wanaolenga kujipatia kipato pasi kujali usalama wa taifa lao. Si mara moja wala mbili ambazo tumesikia matukio ya wahamiaji haramu...**

WIZARA ya Mambo ya Ndani nchini kupitia Idara ya Uhamiaji imekuwa ikichukua hatua mbalimbali za kupambana na uhamiaji haramu kama moja ya njia za kukabiliana na uhalifu nchini.

Baadhi ya hatua hizo ni pamoja na misako na ukaguzi wa maeneo mbalimbali ikiwamo nyumba za kulala wageni na katika vyombo vya usafiri pamoja na udhibiti wa mipaka katika ya Tanzania na nchini jirani.

Misako na udhibiti huu umekuwa ukisaidia kukamatwa kwa wahamiaji katika maeno mbalimbali wengi wao wakiwa wanaitumia Tanzania kama njia ya kwenda katika mataifa mbalimbali hususani yale ya Kusini mwa Afrika kwa lengo la kusaka maisha bora.

Kwa kiasi kikubwa wanaowasafirisha wahamiaji hawa wanatajwa kushirikiana na Watanzania wasiokuwa waaminifu, wanaolenga kujipatia kipato pasi kujali usalama wa taifa lao.

Si mara moja wala mbili ambazo tumesikia matukio ya wahamiaji haramu wakikamatwa wakisafirishwa huku wakiwa wamefichwa katika magari ya mizigo bila hata kujali usalama wa afya zao.

Kutokana na kukomaa kwa biashara hii serikali iliamua kutunga sheria kali za kudhibiti uhamiaji haramu ikiwamo kutaifishwa kwa magari yanayotumika kuwasafirisha au nyumba ambazo zinatumika kuwahifadhi.

Pamoja na jitihada zote hizi bado hazijazaa matunda ya kukomesha biashara hii ambayo karibu kila mwezi vyombo vya habari vinaripoti taarifa za wahamiaji haramu na hata wiki hii taarifa zimeripotiwa.

Binafsi macho yangu yameona liko tatizo la ukosefu wa elimu ya kutosha katika jamii kuhusu madhara ya biashara hii inayoendelea kushamiri nchini.

Nasema elimu kuhusu madhara ya biashara hii haramu inapaswa kutiliwa mkazo zaidi ili kuiwezesha jamii kuona iko haja ya kuachana na biashara hii na kutambua umuhimu wa kutowahifadhi wakimbizi na kufahamu athari zake kijamii na kiuchumi.

Nasisitiza kuwa elimu hii ni muhimu kwa kuzingatia Tanzania inatajwa kuwa njia kuu ya wahamiaji haramu katika ukanda huu wa Afrika Mashariki na kwa kuzingatia kuwa ndiyo nchi pekee katika ukanda huu iliyopakana na nchi nyingi zaidi.

Kutolewa kwa elimu kuhusu uhamiaji haramu kutawezesha wananchi kutoa taarifa katika vyombo vya dola pale wanapoona watu wanaowatilia shaka kuwa si Watanzania. Pia itasaidia raia kutowahifadhi wahamiaji haramu ambao ni hatari katika ustawi wa taifa letu.

Ikumbukwe kuwa ni rahisi kwa mgeni kutenda tukio na kuondoa katika eneo hilo na kukimbilia nchini mwake na asipatikane, hivyo kuwahifadhi kunaweza kusababisha uvunjifu wa amani na uporaji wa rasilimali za nchini.

Kuendelea kuwahifadhi wahamiaji haramu kutaweza pia kuhatarisha maeneo tengefu na hifadhi mbalimbali kwa kuyafanya kuwa malisho ya mifugo hasa kwa wahamiaji haramu wanaoingia nchini kwa lengo la kutafuta malisho ya mifugo yao hasa kwa mikoa ya mipakani.

Nashauri kuwa elimu hii haipaswi kuishia kutolewa katika vyombo vya habari pekee ambavyo si wote wanapata fursa ya kuvisikiliza kutokana na majukumu mbalimbali.

Iko haja sasa ya kutumia njia za ujumbe mfupi wa maandishi wa kueleza athari za kuwahifadhi wakimbizi katika jamii ikiwamo uporaji wa ajira ambazo kimsingi hupaswa kuchukuliwa na wazawa.

Kwa sababu kuona ni kuamini basi Idara ya Uhamiaji iwe na utaratibu wa kuendesha mikutano katika maeneo ya vijiji vya mipakani ili kuwaeleza wananchi kuhusu hatari ya kuwahifadhi wakimbizi.

**Mungu ibariki Tanzania**

**Kwa maoni na ushauri tumia barua pepe mwanakatwe2015@gmail.com**

## DARASA LA NDOA

# Dhana ya upendo wa dhati katika ndoa



Na Mch.Dk. Enock Mlyuka

**Mwenzi mwenye upendo wa dhati hushauri na kuonesha moyo wa uvumilivu, kwani ubora wa mwenzi hubebwa na kasoro za mwenzi wake. Hii ina maana kuwa, mwanandoa huongeza thamani na kuonesha ubora wake pale anapofanikiwa kumsaidia mwenzi wake katika udhaifu alionao. Mwenzi mwenye upendo wa dhati hushauri bila kuchoka na kumwomba Mungu ili ashughulike na udhaifu wa mwenzi wake.**

NDOA ni taasisi ya kwanza ya kijamii Mungu aliyoianzisha hapa duniani. Taasisi hii ili idumu inahitaji malezi ya mume na mke. Upendo wa dhati unapokuwapo huchangia katika malezi bora ya ndoa. Upendo hauji kimiujiza bali hutengenezwa. Upendo katika ndoa hutengenezwa kwa matendo na kauli njema za mwenzi. Kwa mantiki hii, ni muhimu kila mwanandoa kuangalia mambo anayomtendea na kumnenea mwenzi wake. Swali la msingi la kujiuliza ni hili, je, umeweka alama gani katika maisha ya mwenzi wako? Je, kauli na matendo yako kwa mwenzi wako ni baraka au karaha?

Mwanandoa mwenye upendo wa dhati atamtendea na kumnenea mambo mema mwenzi wake. Upendo ni kutenda wema na kunena mema juu ya binadamu mwingine. Mwanandoa mwenye kutenda wema hukataa roho ya ubinafsi na kiburi, bali hutanguliza mahitaji na kujali hisia za mwenzi wake. Penye upendo wa dhati pana kujengana, kuimarishana, kushirikiana, kusaidiana, kutunzana, kuchukuliana, kuheshimiana, na kusameheana ili kufikia malengo na mafanikio ya ndoa.

Mwenzi mwenye upendo wa dhati hushauri na kuonesha moyo wa uvumilivu, kwani ubora wa mwenzi hubebwa na kasoro za mwenzi wake. Hii ina maana kuwa, mwanandoa huongeza thamani na kuonesha ubora wake pale anapofanikiwa kumsaidia mwenzi wake katika udhaifu alionao. Mwenzi mwenye upendo wa dhati hushauri bila kuchoka na kumwomba Mungu ili ashughulike na udhaifu wa mwenzi wake.

Upendo wa dhati ni kizuizi cha hasira na maamuzi hatarishi. Upendo wa dhati humsukuma mwanandoa kufikiri athari za hasira na maamuzi yake juu ya mwenzi wake. Upendo wa dhati huleta utu katika hushughulika na migogoro. Upendo wa dhati hauweki vinyongo na kumbukumbu za makosa wala kulipiza visasi, bali humsukuma mtu katika kusamehe makosa na kuendeleza maisha.

Upendo wa dhati huvutia tabia ya kupenda kusema ukweli kwa kuwa ukweli hutuweka huru na udhalimu. Ukweli ni chimbuko la haki katika maisha. Pamoja kwamba ukweli unauma, lakini ukweli ni dawa ya nafsi iliyojeruhiwa na yenye kutamani mambo mema. Hivyo, wanandoa wajifunze na kupenda kuelezana ukweli kuhusu maisha na matamanio yao. Kuweka mambo moyoni hakuleti tija bali hubomoa afya na maisha.

Siku zote upendo wa dhati huleta ulinzi (protects). Upendo wa dhati humsaidia mwenzi kujisikia yuko salama katika uhusiano wake wa ndoa; humlinda dhidi ya vitendo vya ukatili na kuleta msukumo wa kutenda mema. Upendo wa dhati husimika uhusiano wa wanandoa na kuwafanya kuwa wamoja zaidi.

Upendo wa dhati huleta tumaini (trust) na uhai wa ndoa. Wanandoa wanaopendana huaminiana. Kutokuaminiana katika ndoa huleta hofu na mashaka ambayo humuondolea mwenzi hali ya kujiamini. Chochote kinachopita mbele yake ataona anaibiwa au anasemwa yeye. Maisha yenye hofu na mashaka husababisha utumwa na hudhoofisha afya ya mwili na akili.

Upendo wa dhati huleta matumaini (hopes) kuhusu maisha. Siku zote upendo huu huleta msukumo kwa mwenzi wa kuona mbele zaidi au mema yajayo. Kuruhusu fikra zetu kuona mambo katika mtazamo chanya na mwanzo wa kuruhusu maisha yenye ushindi na mafanikio ndani yetu. Wanandoa wanapokuwa na mtazamo chanya kuhusu maisha yao wanakuwa wamechagua amani na furaha kuingia ndani yao.

Maisha ni pamoja na utamu na uchungu. Upendo wa dhati haushindwi na lolote hata pale yanapotokea mabadiliko katika maisha. Mwanandoa mwenye upendo wa dhati huwa hakimbii matatizo, bali humtia moyo na kumfariji mwenzi wake wakati wa huzuni na changamoto.

Kila ndoa hupitia hatua mbalimbali za maisha. Hatua hizo na mabadiliko yanayotokea ndio yaletayo changamoto. Kila ndoa nzuri imepitia changamoto. Kwa hiyo, wanandoa wawe tayari kuzikabili changamoto na kuyapokea mabadiliko. Upendo wa dhati wa mwenzi huonekana na kuthibitishwa wakati wa changamoto. Uwapo wa mwenzi uonekane katika raha na shida. Ndoa zilizodumu na zenye furaha ni zile ambazo changamoto zilipotokea, wanandoa walizikabili kwa pamoja.

[Dk. Mlyuka ni mchungaji wa KKKT na Mkurugenzi Mtendaji wa Tanzania Marriage and Child Care Foundation (TaMCare), asasi inayojishuhulisha na masuala ya ndoa, familia na malezi. Kwa maelezo zaidi, tembelea www.tamcare.or.tz. Fuatilia mafunzo zaidi katika tamcaretv online. Kwa maoni na ushauri wasiliana naye kwa: info@tamcare.or.tz

**Mwenzi mwenye upendo wa dhati hushauri na kuonesha moyo wa uvumilivu, kwani ubora wa mwenzi hubebwa na kasoro za mwenzi wake. Hii ina maana kuwa, mwanandoa huongeza thamani na kuonesha ubora wake pale anapofanikiwa kumsaidia mwenzi wake katika udhaifu alionao. Mwenzi mwenye upendo wa dhati hushauri bila kuchoka na kumwomba Mungu ili ashughulike na udhaifu wa mwenzi wake.**

# MAISHA

JUNI 6, 2021

Nipashe

Baba, Mama na Mwana

*Jumapili*



Ukurasa 14

## Kisamvu cha nazi



Ukurasa 15

## MAISHA NI NYUMBA

Nyumba imara huhimili vishindo vingi



## HARUSI

Ukurasa 12




USIJIKANDIKE 'MAKE UP'


# Fuata njia hizi utaonekana mrembo

Ukurasa 14

# TOA TOFAUTI 5



## FUMBO TOTO



Jaza maneno yafuatayo katika vyumba vilivyopo wazi:
ULAJI, ANA, SAA, UKUTA, APIZA, SHABA

## AMSHA AKILI




## WATOTO

# PAKA RANGI



@MSAMBA

## CHEKA



Alichokifanya daktari

Ebu angalia jamaa mroho alimtembelea rafiki yake na alipofika alikaribishwa ugali na nyama nyingi tu. Wakati anakula akagundua kuwa shemeji yake, mke wa rafiki yake hali nyama.

**JAMAA:** Aise hili ni bonge ya lanchi, lakini mbona sisi tu tunakula nyama shemeji hali kabisa anaishia mchicha tu?

**RAFIKI:** Hapana sijamkataza, ila shemeji yako halagi nyama ya fidi kama sisi.

**JAMAA:** Duuu sitaki tena chakula chenu, umesikia mimi nakula fisi?

**SWALI**

Mto Ruvuma unapatikana upende gani wa Tanzania?

## MAISHA NDIVYO YALIVYO
Na Flora Wingia



# Kutokuwa nguvu ya kumiliki kunavyoweza kutesa wengi!

KARIBU tena msomaji tuendelee na mada zetu kuhusu Maisha Ndivyo Yalivyo. Bado nipo katika anga la vijana na changamoto za kimaisha walizo nazo, lakini hawajui watokeje hapo. Nimeeleza mara nyingi hapa kwamba hakuna jambo linalotokea pasipo chanzo.

Wiki iliyopita nilimjadili kijana ambaye aliamua kujiajiri kwa kuingia kwenye biashara ya usafiri wa bodaboda.

Alianza vema akapata abiria kila aliporudi kituoni. Hali hiyo iliwashangaza wenzake ambao hawakuelewa ni kwa nini kijana huyu alikuwa na mvuto wa abiria kuliko wao.

Ikawa imepita takriban miezi mitatu, huku kipato cha kijana kikiongezeka kupitia bodaboda yake hiyo mpya, ghafla hali ikabadilika. Kijana anapokuja kituoni, akipata abiria akapanda, anateremka kwa madai ananuka.

Akawa hapati tena abiria na hata wenzake wanamtenga eti ana harufu mbaya akiwa karibu nao. Ndipo akaamua kubakia nyumbani haendi tena kazini. Mama yake akimuuliza anamwambia wenzake wanasema ananuka na hata abiria hawamtaki tena. Lakini cha ajabu awapo nyumbani hana harufu yoyote.

Hicho ni kisa nilikinasa nikiwa Morogoro hivi karibuni kwa kusimuliwa na mama yake mzazi. Kijana mmoja naye huko Kigamboni Dar es Salaam akanipigia kuelezea anguko lake. Alikuwa ameinuka kiuchumi hata kufikia hatua ya kumiliki kiwanda. Lakini madeni yakamzidi akakifunga na sasa ana duka dogo la nguo za watoto.

Mpenzi msomaji, ukiona mtu anafanikiwa, ana nguvu. Ukiona biashara ya mtu inasitawi, huyo mfanyabiashara ana nguvu. Ukiona mtu amepandishwa cheo, ujue ana nguvu. Hata hivyo, inawezekana ikawa ni nguvu nzuri au mbaya.

Maandiko ya Mungu yamewekwa bayana kwamba unapotii sheria na amri zake atakubariki, atakuzidisha pamoja na uzao wako kama nyota za mbinguni na kama mchanga wa pwani. Na uzao wako utamiliki mlango au malango ya maadui zako.

Mungu anajua kwamba kila mwanadamu anayetaka kuinuka juu kimafanikio, ipo vita mbele yake. Kumiliki ni nguvu. Kama huna nguvu huwezi kumiliki. Na siku zote mwenye nguvu atammiliki asiye na nguvu. Hiyo ni kanuni ya ulimwengu wa roho.

Kumiliki ni kitu gani? Ni kuwa nacho, kuwa na mamlaka, kuwa na nguvu juu ya jambo fulani au juu ya watu fulani. Kuwa nacho kwa kumiliki nyumba, gari, mashamba, kiwanda na kadhalika. Mtu asiye na nguvu ya kumiliki, hana anachomiliki. Maisha Ndivyo Yalivyo!

Huwezi kumiliki kitu kama huna nguvu katika ulimwengu wa roho. Ukimuona mtu biashara yake inachanganya kwa kuuza, huyo ana nguvu katika ulimwengu wa roho. Ukiona mtu anaishi na mume wake vizuri ni kwa sababu ana nguvu ya kumiliki mwanamume.

Ukiona unashindwa kummiliki hata mke wako, elewa kuwa una shida. Yaani ukitoka na yeye anatoka, akienda naye anakwenda na ukirudi naye anarudi. Inakuwa kama vile mchezo wa kuigiza, lakini ni maisha halisi ya watu hao.

Kuna watu wameshindwa hata kumiliki wachumba. Anachumbiwa na huyu leo anashindwa kummiliki anatoka na kwenda kwa mwingine. Mchumba wa kwanza, wa pili na hata watatu wote wameondoka. Jiulize, tatizo ni nini? Jibu ni kwamba huna nguvu ya kumiliki.

Na hao wanaokuponyoka kule waendako wanatulia. Matokeo yake unaweza kudhani kuwa wale waliowachukua na kudumu nao walikuonea wivu au walitumia nguvu za giza. Hilo nalo linawezekana, lakini kutokuwa na nguvu ya Mungu ya kumilikiki ni kigezo muhimu sana.

Huhitaji nguvu za mwili zitokanazo na lishe ili uweze kumiliki, bali nguvu za kiroho. Ukiwa kazini kama huna nguvu ya kumiliki lazima bosi wako atakunyanyasa. Lakini ukiwa na nguvu atakufurahia. Kadhalika kwa wafanyakazi wenzako. Maisha Ndivyo Yalivyo!

Tafuta nguvu ya Mungu kumiliki. Pale wenzako wanafukuzia nguvu za giza kufanikiwa, wewe mtumaini Mungu kwani ni mpaji wa vyote, muweza wa yote hajawahi shindwa lolote. Nguvu ya kumiliki yatoka kwake kinyume cha hapo tegemea anguko.

***Mpenzi msomaji, bila shaka lipo jambo umejifunza hapo. Tumuombe sana Mungu atupe nguvu ya kumiliki. Niishie hapa kwa leo. Je, una maoni, au kisa cha kimaisha? Tuma ujumbe mfupi kupitia 0715268581.***

## NAWAZA KWA SAUTI
Na Salome Kitomari



# Utoaji huduma hospitali za umma umulikwe

***WIKI iliyopita Rais Samia Suluhu Hassan, alifanya ziara ya kushtukiza maeneo manne ikiwamo Hospitali ya Rufaa ya Mwananyamala, Dar es Salaam ili kujionea utoaji wa huduma.***

Ziara hiyo ilituma salamu kwa watendaji wa umma kuwa wanapaswa kuwajibika ipasavyo katika kutekeleza majukumu yao kwa kuwa serikali iko macho na inafuatilia kwa karibu.

Napongeza kwa hatua hiyo ambayo huenda itasaidia kuwashtua watendaji kuwa serikali iko macho na wakati wowote Mkuu wa nchi anaweza kufika kwenye eneo lao na kujua yanayoendelea, maana yake kinachotakiwa ni uwajibikaji. Pamoja na jitihada hizo ambazo zimekuwa zikifanywa na viongozi wa kiserikali wa ngazi nyingi, lakini bado ipo haja ya kumulika sana hospitali za umma.

Leo nitazungunzia Mwananyamala ambayo nimewahi kipeleka mgonjwa, kilichonikuta na majibu niliyopata baada ya kudodosa kwanini hali iko hivyo, na hii ni mfano halisi ikiwa ni moja kati ya wengi wanaotendewa hivi.

Nilipeleka mgonjwa ambaye alijifungua siku chache zilizopita hospitalini humo na kupata shida ya nyonga, nilivyofika nilichukua kiti cha wagonjwa na kutakiwa kuinua mgonjwa wangu na kumkalisha.

Nilifanya hivyo kwa shida sana kwa kuwa ni mtu mzima hivyo ni ngumu kumuinua mwenyewe, nilimuomba mpita njia anisaidie katika hilo. Nilivyofika mapokezi kwanza nilikutana na majibu ilimradi na hiyo ni kutokana na ugeni wangu katika kujua wapi pa kuanzia, niliandikiwa kwenda kumuona daktari.

Nilivyofika chumba cha daktari hakuwapo nililazimika kusubiri kwa muda na alivyokuja nilijua natakiwa kuingia, lakini nilifukuzwa kwa lugha kali ya "subiri huko nje hadi nikuite" ilichukua tena muda flani hadi kuingia ndani.

Nilipoingia kwa kuwa mgonjwa wangu hakuwa anajiweza nilitakiwa kumpandisha kitandani na nilivyoona siwezi niliomba msaada wa daktari ambaye alijibu ovyo kuwa "Kama hutaki atibiwe utajua mwenyewe ila hakikisha anapanda hapo kitandani." Na haikutosha alimtaka asimame wakati mgonjwa alikuwa hawezi hata kujisogeza mguu na aliposema hawezi kunyanyuka alimfuata na kumminya nyonga kwa nguvu (mtu mwenye hasira kali).

Tulipambana mimi na mgonjwa wangu ili kumpandisha kwenye kitanda kwa ajili ya uangalizi, baada ya hapo tulitakiwa kwenda kupiga X-Ray, ambayo katika chumba tuliwakuta vijana wenye morali na walinisaidia kumnyanyua mgonjwa na kumpandisha kitandani.

Baada ya X-Ray nilitakiwa kurudi kwa daktari na nilipofika mlangoni tu nakutana naye anatoka na kututaka turudi siku ya Jumatatu, wakati huo mgonjwa anaumwa sana hata hawezi kufanya lolote, na baada ya kulalamika tulipewa panadol za kutuliza maumivu.

Nilijiuliza sana kwamba ni wagonjwa wangapi wanakwenda hapo na kupata huduma za aina hiyo, kwamba kuanzia mapokezi kwenye kulipia lugha ni mbaya, ukifika kwa daktari naye hali hiyo hiyo na mwisho unaondoka na maumivu au ugonjwa wako.

Nikiwa hapo nilivutiwa kuuliza kwanini hali iko hivyo kwa kuwa binafsi nimezoea kutibiwa hospitali binafsi ambazo mgonjwa ni mteja hivyo wanamjali kwa kuhakikisha anapata huduma zote muhimu tena kwa ubora. Nilizungumza na kijana aliyekuwa maabara na dada mwingine aliyekuwa mapokezi, swali langu kwao ilikuwa mbona kila mfanyakazi anaonekana ana kisirani katika kuhudumia, kwani kuna shida gani.

Ndipo walipofunguka kwa nyakati tofauti kuwa dada usitutone hivi kali zetu ni ngumu hakuna motisha, hakuna malipo ya muda wa ziada, tuna malimbikizo mengi, maisha yetu ni magumu, mfano daktari aliyekuhudumia huenda hata hajui nyumbani kwake watakula nini, hivyo wewe tusamehe tu ridhika na hata hii huduma uliyopata maana nasi tuna matatizo yetu mengi kubwa mishahara ni midogo sana.

Nilishtuka kwa kuwa huyo ni mmoja na daktari alinionyesha kwa vitendo hakuwa tayari kuzungumza, nilichokifanya sikurudi tena hospitalini humo badala yake nilimtafuta daktari hospitali binafsi ambaye aliniandikia dawa za kununua na mgonjwa wangu alipona kabisa.

Kwa kawaida mtu anapokuwa mgonjwa anapofika hospitalini akimuona daktari anapata tumaini la kupona kabla hajahudumiwa, hiyo inategemea na jinsi alivyompokea na kumpa huduma, inapokuwa tofauti ni kumuongezea mgonjwa matatizo.

Juzi, katika moja ya kundi letu la taaluma mmoja wa mwanataaluma ameeleza yaliyomkuta baada ya kwenda hospitalini humo akisumbuliwa na mifupa, na aliishia kufukuzwa na daktari hadi alipowasiliana na watu Wizara ya Afya ndipo akapata huduma.

Anaeleza kuwa daktari anayemhudumia siku zote ndiye huyo, lakini alimbadilikia akamjibu vibaya na kumtoa ndani ya chumba. Hii ni mifano michache kati ya mingi, wangapi wanakosa huduma au kupewa huduma ovyo kwa mazingira kama haya, mbona haya hayafanyiki kwenye hospitali binafsi, na je, nini kinafanyika kuweka morali na kuboresha utendaji kazi kwa hospitali inayohudumia mamia ya watu?

Ipo haja kwa serikali kufuatilia kwa karibu sana kero na huduma hafifu zinazotolewa, ipo haja ya kuzungumza na wafanyakazi na kuwapa morali, maana kama hospitali ya mjini hali iko hivi, vipi hospitali, vituo vya afya na zahabati huko vijijini?

Hii inatuma salamu kuwa kuna umuhimu mkubwa wa kuiangalia sekta ya afya, kuangalia namna ya kuwafanya wafanyakazi wajifunze yanayofanyika sekta binafsi ili siku moja huduma kwenye hospitali za umma iwe bora zaidi ya sekta binafsi.

***Mungu ibariki Tanzania***

# HARUSI





Ilikuwa siku ya furaha kwa Robin Talemwa Gideon na Winnfrida Emmanuel Macha baada ya kufunga katika kanisa la Katoliki la Kristo Kuhani Mkuu wa Milele Mei mosi, jijini Mwanza na kufuatiwa na sherehe ya kuwapongeza katika ukumbi WA Gold Crest.









# MITINDO



STARA FASHION 2021

# Furahia 'Uhuru' kuvaa

HATIMAYE onyesho la saba la Wiki ya Mitindo ya Stara, limepangwa kufanyika Julai 30 jijini Dar es Salaam.

Jukwaa hilo la mitindo lenye kaulimbiu 'Uhuru' litawakutanisha wabunifu 20 mahiri kutoka mikoa ya Arusha, Morogoro, Dodoma na Zanzibar.

Mbali na maonyesho ya jukwaani hafla hiyo pia itakuwa na vibanda vya wabunifu, na bidhaa zinazopatikana kwa ununuzi, Mwandaaji wa onyesho hilo, Latifah Makau, amesema kutakuwa na semina na mikutano ya awali ili kuwatayarisha wabunifu kiuweledi.

"Wiki ya mavazi ya Stara itapambwa na mitindo huru itakayoenzi tamaduni mbalimbali Duniani kote," amesema.

Onyesho hilo litafanyika katika Mgahawa wa flava iliyoko Masaki kuanzia asubuhi hadi jioni kwa maonyesho ya bidhaa na saa 10 jioni itakuwa mitindo ya jukwaani

"Katika jitahada zetu za kuunga mkono nguvu ya mitindo kushawishi, tulifikiri itakuwa busara kutumia jukwaa letu kukuza uelewa wa mambo mbalimbali na labda kuanza kuwa mabadiliko ambayo tunataka kuyaona," ameongeza Latifah.

Waandaaji pia wanatoa nafasi ya kuunganisha watengenezaji wa mitindo na ulimwengu wa mitindo na watu maarufu.


Maonyesho haya pia yanatazamiwa kujumuisha sanaa ya henna na Mapishi. Baadhi ya wabunifu mashuhuri waliojitokeza kushiriki ni wabunifu wa chapa ya BK, Pichichii, Sayshan AB design na wengine wengi kutoka Tanzania ..

Toleo la mwaka huu limedhaminiwa na karakana ya Nzowa Auto, Express ndogo, wasambazaji wa vifurushi na kampuni ya suluhisho za kidijitali za Ian Ads Unidots, Marashi Zanzibar, Coca Cola Tanzania, Mozen Threading, kati ya kampuni zingine. Kampuni ya usambazaji limited Express imedhamiria kusaidia wabunifu na wajasiriamali.









## UREMBO



### USIJIKANDIKE 'MAKE UP'

# Fuata njia hizi utaonekana mrembo

SUALA la kujiremba kwa vipodozi ni jambo la kawaida kwa kila mwanamke anayejipenda.

Mwanamke anayejiamini anahitaji kila siku kuwa na mwonekano tofauti kuanzia umbo, nywele hadi sura.

Kujiremba sura maarufu kama 'Make up' ni jambo linalowekwa umuhimu kiasi ambacho watu wanajikusanyia pesa nyingi kutokana na mahitaji kuwa makubwa.

Hata hivyo, kujiremba uso kupitia watoa huduma hiyo mitaani ni gharama kubwa, kuliko ukifanya wewe mwenyewe ukiwa nyumbani kwako.

Leo utapewa vitu muhimu vya kukaa navyo nyumbani ili kila unapohitaji kujipodoa uso, basi inakuwa rahisi kufanya hivyo.

**PRIMER**

Kipodozi hiki unatakiwa kuwa nacho, kinafanya kazi kwa kupaka usoni baada ya mafuta ya kulainisha ngozi aina ya losheni.

Kazi yake kubwa ni kuzia vipodozi vikae usoni muda mrefu na inaziba matundu na madoa kwenye ngozi.

**CONCEALER**

Kazi yake ni kuziba madoa yasiyopendeza usoni na kufanya ung'ae pamoja na kurekebisha wanja unyoke.

**FOUNDATION**

Foundation huwa katika aina tofauti ,kama vile poda, krimu au kimiminika. Kazi ya kipodozi hiki ni kufanya uso kuwa mnga'vu na laini. Foundation hutumika kwa kupakwa kwa kutumia brashi,sponji au penseli.

**EYE SHADOW**

Hii inapakwa kwenye ngozi ya Juu ya jicho. zipo za rangi nyingi na unapaka kulingana na unavyopenda wewe.

**EYE LINER**

Eye Liner inapakwa kuzunguka jicho ili kulipa mwonekano mzuri.

**WANJA**

Pia weka wanja kiasi, unaweza kutumia ule wa penseli au wa lulu.

**BLASHI NA BRONZER:**

Hupakwa kwa mbali kwenye mashavu ili kuyapa mng'ao wa kipekee.

**LIP LINER**

Hii inapakwa kando ya midomo ili rangi ya midomo (Lipstick)' kae vizuri

**RANGI YA MIDOMO (LIP STICK)**

Rangi ya midomo ipo ya rangi mbalimbali, unaweza kuchagua rangi unayoipenda kwa ajili ya kupaka. Pia kuna za mafuta na kavu, hivyo uhuru ni wako.

Kumbuka baada ya kukamilisha unaweza kupaka mafuta ya mdomo, na ukamalizia kwa kupaka poda kiasi ili kuwa na mwonekano mzuri.



## MAPISHI

Na Mary Geofrey



# Kisamvu cha nazi

KISAMVU ni mboga tamu inayofaa kuliwa na ugali na wali. Kisamvu kilichokolea nazi hakiishi utamu wake hasa ukila na wali.

**MAHITAJI**

Kisamvu kilaini, kitunguu maji, kitunguu swaumu, chumvi, nazi mbili zilizokomaa vizuri.

**NAMNA YA KUANDAA**



Chambua kisamvu na utwange kwenye kinu ukichanganya na vitunguu saumu mpaka kiwe laini, kuna nazi laini na uchuje tui zito na jepesi.

Menya na twanga vituu swaumu, uchanganye na kisamvu chako na ubandike jikoni kichemke mpaka kilainike.

Wakati kisamvu chako kinachemka anza kukatakata vitunguu maji vipande vidogo na anza kupika kisamvu chako hadi kiwe laini.

Kisamvu kikishaiva na maji kukauka, weka kitunguu maji na chumvi, kisha weka tui jepesi ili kiiendelee kuiva zaidi na kuwa laini.

Tui likikauka kabisa weka tui zito na pika hadi tui likauke kubaki na mchuzi kidogo.

Unaweza kujiramba na mapishi yako kwa kula kisamvu chako na wali.

MAISHA NI NYUMBA

Na Elizabeth Zaya

# Nyumba imara huhimili vishindo vingi





UIMARA wa nyumba ni kuhimili mambo mengi ikiwamo changamoto zinazojitokeza katika nyakati za mvua, upepo mkali pamoja na uzito wowote unaoipiga.

Peter Akoye, anayejishughulisha na masuala ya ujenzi wa nyumba, anasema uimara na uzuri wa nyumba unategemea vitu vingi.

Kwamba, kwa nyumba za kawaida, uimara wake huanzia kwenye ujenzi wa msingi, kuta, paa, nguzo, mihilimi, milango, madirisha, dari ambayo yote haya yanapaswa kuzingatiwa wakati wa ujenzi wake.

"Nyumba imara na mwonekano mzuri ni alama kwa eneo husika, huongeza thamani ya jengo, mandhari ya jengo iliyowekwa katika uzuri, pia huleta hisia na utulivu, furaha na uchangamfu kwenye familia na mtaa," anasema Akoye.

"Ni muhimu jengo liwe imara na uzuri unaoendana na matumizi yake, kama ni kwa ajili ya biashara, basi liwe lenye mvuto hata wateja, kama ni kwa ajili ya kuishi familia, basi ichangie kuleta amani na furaha nyumbani."

Anashauri kwamba ni vyema nyumba ikafanyiwa usanifu mzuri na bora kuanzia jengo lenyewe, mazingira ya ndani, mandhari ya nje ili yabebe maana fulani na kwamba ni muhimu kuwa makini na maana hiyo unayomwambia mtu kupitia nyumba yako.

"Rangi, mpangilio, mpishano, kimo, ukubwa, umbile la nyumba yako huathiri hisia za mtumiaji. Pia niwakumbushe kwamba rangi nyeupe kwenye nyumba huleta hisia za usafi, utaratibu na amani."

"Kijani huleta hisia za utulivu, uasili. Nyekundu huleta hisia za kusisimua, shauku, changamfu. Rangi ya waridi huleta hisia ya furaha na ya bluu huleta hisia za uasilia na utulivu pia, kwa hiyo ni muhimu kufanya chaguo sahihi unapopanga au unapokamilisha ujenzi wa nyumba ya ndoto yako."

Anashauri kwamba jambo la msingi ni kujenga nyumba unayohitaji, itakayokidhi mahitaji ya sasa na baadaye, yenye usalama na uimara, iliyo katika uzuri wake na kuepuka kujenga usiyoihitaji.

Kufahamu aina ya nyumba inayokufaa kujenga ni miongoni mwa jambo linalosisitizwa na mtaalam huyu kwa kuwa ndiye mahali muhimu ambapo kila mtu anapatia faraja na kupata muda wa kupumzika baada ya shughuli nyingi za kujitafutia kipato.


## Dondoo muhimu namna ya kuchagua taa za kuweka kwenye dari ya sebule yako

**1:** Chagua rangi ya taa unazotaka ziwe juu ya dari yako, hakikisha taa zisiwe na mwangaza mkali ili kuweka sebule katika muonekano mzuri.

**2:** Angalia aina ya urembo unapenda wa kifaa cha kuning'inia juu ya dari, wengi wanependa muonekano wa mishumaa au yai.

**3:** Unaweza kuweka taa za kawaida lakini zina kiwambo cha kung'arisha eneo pana.

**4:** Unaweza kuweka taa za mikanda kuzunguka maua ya dari yako ili kukupa mwanga na mapambo ndani ya sebule.





# KATUNI

## KATUNIKA KI'DOMOKRASIA


BY ABDUL KINGO - 2021

SMS - 0621 412 879











## JUKWAANI










*KINYUNYIZO CHA LEO... ...MNUNIE BOSI UPATE BANDO LA NJAA

# Nigeria yaifunga Twitter

**ABUJA,** NIGERIA

SERIKJALI ya Nigeria imeufungia mtandao wa kijamii wa Twitter kupitia simu za mikononi katika miji ya Logos na Abuja.

Hatua hiyo imechukuliwa baada ya serikali kutangaza kwamba itafungia bila kikomo huduma za Twitter nchini humo.

Taarifa iliyotolewa na Waziri wa Mawasiliano wa Nigeria, Lai Mohamed, ilisema serikali ilisema marufuku hiyo imetokana na kuongezeka kwa matumizi ya mtandao na kutishia usalama na umoja katika nchi hiyo.

Hata hivyo, Twitter ilisema tangazo hilo nimewasikitisha.

Kuanzia jana asubuhi, raia wa miji hiyo walisema wameshindwa kupata mtandao huo kupitia kampuni mbili za simu za MTN na Airtel.

Hata hivyo, Twitter inapatikana kupitia mitandao mingine ya wi-fi , lakini njia hiyo ni ngumu kupata intaneti nchini Nigeria.

Watu wanajaribu kutumia visaidizi vya kupata huduma ya Intaneti kama "VPN" ambayo imepata umaarufu ghafla, kulingana na mtandao wa Trendsmap ambao unafuatilia masuala ya mitandaoni.

Serikali ya Nigeria ilikasirishwa baaada ya ujumbe wa Rais Muhammadu Buhari, kuondolewa Twitter kwa kukiuka kanuni za mtandao huo.

Rais Buhari ambaye aliwahi kukosoa hatua ya mtandao huo mkubwa wa kijamii wa Marekani kuondoa ujumbe wake, na kuutaja kuwa ni upendeleo.

Ujumbe uliotumwa na kiongozi huyo Juni mosi, ulielezea vita vya Nigeria vya wenyewe kwa wenywe mwaka 1967-70 na kuwaonya wale wanaofanya vibaya leo kwa kutumia lugha ambayo wataielewa.

Msemaji wa Twitter, alisema wakati ujumbe huo ulipotumwa ulikiuka Sheria.

Kampuni hiyo hiyo ambayo mwezi Aprili ilitangaza makao yake makuu mapya barani Afrika itakuwa nchi jirani ya Ghana , ilisema inachunguza na itatoa taarifa wakati itakapopata maelezo zaidi.

**BBC**



Wanajeshi wa BurkinaFaso wakilinda moja ya eneo linaloshambuliwa mara kwa mara na wanamgambo wa makundi yenye misimamo mikali ya Al-Qaeda na ISIL **PICHA: AFP**

# Rais Putin aikemea Marekani

**MOSCOW,** URUSI

RAIS wa Urusi Vladmir Putin, ameishutumu Marekani kwa kujaribu kuikandamiza nchi hiyo.

Kauli hiyo kali ameitoa wakati anajiandaa kukutana na Rais wa Marekani, Joe Baden, katika kikao kinachofanyika leo.

Akizungumza wakati wa mkutano wa kiuchumi mjini St. Petersburg, Rais Putin, alisema udhibiti wa silaha, mizozo ya ulimwengu, janga la virusi vya corona na mabadiliko ya tabianchi ni kati ya maswala watakayojadiliana na kiongozi mwenzake wakati wa mkutano huo utakaofanyika mjini Geneva, Uswisi.

Akitumia tukio la uvamizi wa Bunge la Marekani, Januari 6, mwaka huu, ulikofanywa na wafuasi wa aliyekuwa rais wa nchi hiyo, Donald Trump, kama ishara ya undumilakuwili wa mataifa ya Magharibi.

Alisema wavamizi hao hawakuwa wezi wala majambazi, bali watu wenye matakwa ya kisiasa, ambayo hayakusikilizwa.

Hata hivyo, kiongozi hiyo alisema nchi zao mbili zinahitaji kutafuta njia za kurekebisha uhusiano wao uliodhoofika kwa sasa, huku akielezea matumaini ya mkutano huo utapunguza mvutano ulioko kati ya mataifa hayo.

**DW**

# Ulaya yapiga marufuku ndege za Belarus

**BERLIN,** UJERUMANI

Mabalozi wa nchi za Umoja wa Ulaya, wameidhinisha mpango wa kupiga marufuku ndege za mashirika ya ndege ya Belarus kuruka au kutua katika nchi zilizo katika umoja huo.

Hatua hiyo imechukuliwa kama sehemu ya vikwazo vya kiuchumi dhidi ya nchi hiyo, ambayo Mei 23, ililazimisha ndege ya shirika la Ryanair iliyokuwa imembeba mwandishi na mpinzani Rais Alexander Lukashenko, kutua Minsk kwa agizo la kiongozi huyo.

Bila pingamizi kutoka kwa nchi wanachama, hatua hiyo ilianza kutekelezwa kuanzia saa sita usiku saa za Ulaya ya Kati (CET), walisema wanadiplomasia hao.

Umoja wa Ulaya pia unapendekeza, kupiga marufuku, mashirika ya ya ndege kutoka Ulaya kuruka juu ya anga ya Belarus.

Kulingana na Eurocontrol, mamlaka ya Ulaya ya ukaguzi wa safari za ndege, karibu ndege 400 za raia huruka juu ya anga ya umoja huo kila siku.

**RFI**

## UN yatabiri janga la njaa Tigray

**NEWYORK,** MAREKANI

MKUU wa masuala ya kiutu wa Umoja wa Mataifa, Mark Lowcock, ameonya dhidi ya uwezekano wa kutokea baa la njaa katika eneo la Tigray ambalo linakabiliwa na mzozo.

Aidha, maeneo mengine yanayotabiriwa kuwa na janga la njaa ni kaskazini mwa Ethiopia, na kuhatarisha maisha wa maelfu ya watu.

Lowcock, alisema kuwa shughuli za kiuchumi, biashara na kilimo katika eneo hilo, zimeharibika na hakuna huduma za benki wala mawasiliano ya simu.

Katika ripoti iliyotolewa juzi, Umoja huo ulisema tayari imeanza kupokea taarifa za vifo vinavyotokana na njaa. Lowcock aliongeza kuwa watu wanahitaji kuamka na jamii ya kimataifa kuingilia kati na kutoa usaidizi unaojumuisha msaada wa kifedha.

Hakuna anayejuwa ni wanajeshi au raia wangapi waliouawa tangu kuanza kwa machafuko ya kisiasa kati ya serikali ya Ethiopia inayoongozwa na Waziri Mkuu Abiy Ahmed, na viongozi wa jimbo la Tigray .

**DW.**

## Askofu ajiuzulu udhalilishaji watoto

**MUNICH**, MAREKANI

ASKOFU mkuu wa Dayosisi ya Munich na Freising nchini Ujerumani, Kadinali Reinhard Marx, ameomba kujiuzulu katika barua aliyomwandikia kiongozi wa Kanisa Katoliki Duniani, Papa Francis.

Kadinali huyo alieleza katika barua hiyo kwamba madhumuni yake ni kukubali wajibu juu ya kashfa ya udhalilishaji wa kingono uliofanywa na baadhi ya viongozi wa kanisa, aliyoiita kuwa ni maafa.

Alisema kuwa taarifa na uchunguzi wa kipindi cha miaka 10 iliyopita umebainisha kushindwa kwa watu binafsi na makosa ya kitaasisi.

Katika maelezo yake kwa vyombo vya habari, Dayosisi Kuu ya Munich na Freising ilisema Papa Francis, amemtaka Kadinali Marx, aendelee na wadhifa wake hadi hapo Baba Mtakatifu atakapomjibu.

Uchunguzi ulioidhinishwa na Baraza la Maaskofu la Ujerumani na kuchapishwa mwaka 2018, ulionyesha kwamba viongozi wa kanisa 1,670 waliwadhalilisha kingono watoto zaidi ya 3,600 kutoka mwaka 1946 hadi mwaka 2014.

**DW**

SAFU

## MAKALA

# Neno Rais lina athiri tabia ya viongozi



Na Magabilo Masambu

**Hivyo utamaduni huu wa kumwita mwanafunzi rais wa serikali ya wanafunzi iwe ni shule ya msingi, sekondari au Chuo Kikuu huku wanafunzi hao, wakijua dhahiri Rais wa nchi anavyopaswa kuheshimiwa, huathirika kisaikolojia na wao kuona kwamba wanastahiki heshima kama ile anayopewa rais wa nchi.**

HIVI sasa katika nchi yetu, kumekuwa na kasumba moja mbaya sana, kila mtu anapenda kuitwa Rais! Juzi juzi yupo mbunge mmoja aliyetoa hoja hii ya jina la Rais kutotumika kila mahala, katika kitabu changu cha JINSI YA KUJENGA UZALENDO NA UONGOZI TANZANIA NA AFRIKA sura ya tano toleo la mwaka 2016, jambo hili nimelieleza kwa kwa kinaga ubaga zaidi, alipotoa hoja hii watu wengi tumeona ni jambo la kawaida sana, lakini nawaambia jambo la kujiita Rais ni tabia ya watu kujitukuza na kutafuta ukubwa na ufalme wa kuheshimiwa.

Leo hii tuna rais wa bodaboda, rais wa chama cha wapangaji, rais wa wanawake, rais wa shirikisho la mpira na marais wengine wengi. Huu ni ushahidi kwamba watu wetu wengi wanapenda sana vyeo na madaraka makubwa kuliko kuwa viongozi wa kawaida.

Hupenda kujitambulisha kwa majina makubwa ili waogopwe na kupewa heshima kubwa, wakati watu hawa wanapaswa kuwa watumishi. Kwa upande wa shule zetu, hali ni mbaya sana. Mtoto hujenga tabia kutokana na mazingira, ikiwa ni pamoja na yale anayoyasikia na kuyaona yakifanyika na wanajamii.

Hivyo utamaduni huu wa kumwita mwanafunzi rais wa serikali ya wanafunzi iwe ni shule ya msingi, sekondari au Chuo Kikuu huku wanafunzi hao, wakijua dhahiri Rais wa nchi anavyopaswa kuheshimiwa, huathirika kisaikolojia na wao kuona kwamba wanastahiki heshima kama ile anayopewa rais wa nchi.

Baadaye hujenga tabia ya kuwaona wanafunzi wenzao kuwa hawana maana na kwamba, wanastahiki kupigiwa magoti na kutumikiwa. Chakushangaza ni kwamba, hata wanafunzi wenzao huwaona kwamba wako sahihi na wanastahili huduma bora zaidi kama viongozi kuliko wao.

Badala ya kutengeneza viongozi tunatengeneza watawala ambao hupenda mara zote kujitofautisha na wananchi wanao waongoza. Ndiyo maana wanafunzi hao wawapo shuleni, hata kwenye ugawaji wa chakula, huwa wanaona wanastahiki kula chakula kingi na bora zaidi kuliko cha wanafunzi wengine. Ukiwauliza watakwambia "Sisi ni viongozi" Kwahiyo kwa utaratibu huu, tunaanza kutengeneza mafisadi, madhalimu na wahujumu uchumi ndani ya nchi yetu.

Ufisadi na wizi hufunzwa. Njia mojawapo ya kujifunza ni viongozi wanafunzi kujiona bora na kustahiki kupata huduma maalum za kijamii tofauti na zile za wenzao. Kwasababu kijana akiitwa Rais, waziri au mbunge na yeye hutaka kuishi maisha yenye kufanana na nafasi hizo.

Wanafunzi wetu ingeamuliwa kuitwa wenyeviti na viranja, badala ya kutumia majina makubwa huku tukidhani ni sifa, kumbe tuna waharibu kisaikolojia kiasi cha kuwafanya wanajione wao ni watu wakubwa sana kimadaraka.

Ukiuliza kwanini wanafunzi waliamua kubadilishiwa majina ya nyazifa hizo maana zamani tulitumia wenyeviti na viranja utajibiwa "Tumeamua watumie majina hayo, ili wajifunze kwaajili ya baadae pale watakapokuwa viongozi wasiyaone majina hayo ni mageni"

Sababu hiyo ni ya ajabu na ni dhaifu sana. Mtoto haitwi baba au mama ili azoee eti kwamba, atakapokuwa mkubwa na kuwa na watoto azoee kuitwa hivyo. Mtoto anastahiki kubaki kuitwa mtoto. Vijana hawa hujifunza mapema kuwa watawala badala ya kuwa viongozi bora. Utovu wa adabu usiwe msingi wa maisha ya sasa na kesho.

Jina lina nguvu ya kujenga tabia mpya. Ukimpatia mtoto wako jina la Simba, siyo kwamba atakuwa simba ila mtoto huyo kama atazifahamu tabia za simba, ataanza kujifunza kuwa kama simba. Vivyo hivyo ukimwita mtoto wako ng'ombe si kwamba atakuwa ng'ombe, bali kama anamfahamu ng'ombe na anazijua tabia zake ataanza kujifunza tabia hizo na hivyo kuishi kama ng'ombe.

Ndiyo maana katika michezo ya watoto anayeigiza kama ng'ombe utakuta analia kama ng'ombe utasikia akilia Mooooo!!Pia hutembea kwa magoti mfano wa ng'ombe. Kwahiyo jina lina nguvu ya kumfanya mtoto aanze kujifunza tabia mpya ya jina hilo.

Kwa kutambua hilo kipindi cha awali cha uongozi wa Mwl J. K Nyerere, viongozi walitumia majina kama vile, mwenyekiti na katika kutaja jina la kiongozi halikutumika jina la mheshimiwa bali, jina la ndugu lilitumika zaidi.

Ukimwita kiongozi "Mheshimiwa" Hasa hawa viongozi wa chini, maana yake kati yake na wewe anaye kuongoza kunatofauti kubwa. Kwamba yeye ni mheshimiwa na wewe ni mtumwa kwake! Uheshimiwa hubadilisha mpaka tembea na hata ongea ya mtu huonesha hali ya kuridhika kupita kiasi na kuonyesha kwamba hana wasiwasi wowote na kwamba kila jambo liko sawa, huku maisha ya watu yakiwa mabaya zaidi na wala hawazi.

**0689157789**
**magabilomjalifu@gmail.com**

## BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# Remmy alikata rufaa kuambiwa 'mrembo'



Na Adam Fungamwango

**Aliingia nchini akitokea Zaire mwishoni mwa miaka ya 1970, (sasa Congo DR), akiletwa na mjomba wake Mzee Makassy. Hata hivyo alikataliwa kupanda stejini kuimba na wenzake wakidai kuwa sura yake haina mvuto, hivyo atawaharibia. Ikumbukwe kuwa Makassy ilikuwa na waimbaji watanashati sana wakati huo.**

WASWAHILI hawakukosea walipokuja na msemo wa 'duniani kuna mambo.' Ni kweli wakati mwingine duniani hapa utaona mambo yanayostaajabisha.

Wakati kuna watu wenye upungufu wanajitenga na kujiona kuwa hawana hadhi mbele ya binadamu wenzao, wapo ambao huo huo upungufu kwao wanautumia kama fursa ya kujitengenezea kipato na heshima kubwa kwenye jamii.

Kuna watu hapa duniani wametufundisha kuwa binadamu anaweza kuwa na upungufu wa kimaumbile au mwingine unaofanana na huo, lakini kama atatuliza akili huo huo unaweza kumfanya awe 'staa'.

Hivi ndivyo ilivyotokea mwanzoni mwa miaka ya 1990, wakati yalipobuniwa mashindano ya kumtafuta mtu mwenye sura mbaya nchini.

Ni moja ya mashindano ya kukumbukwa na kuacha historia kubwa kwa vizazi na vizazi nchini Tanzania.

Yalifanyika kwenye ukumbi wa Vijana Sochial Hall, Kinondoni. Kabla ya kufanyika, washiriki mbalimbali walijitokeza.

Awali lilichukuliwa kuwa ni la kawaida. Lakini kadri muda ulivyozidi kusonga mbele na kutangazwa sana kwenye vyombo vya habari likawa na mvuto.

Na mvuto uliongezeka zaidi walipojitokeza 'mastaa' wakubwa wawili wakati huo. Mwanamuziki maarufu nchini Dk. Remmy Ongala na msanii wa maigizo, au maarufu wakati huo mchezo wa redio, Bakari Mbelemba, maarufu kama Mzee Jangala.

Maandalizi yalifanyika. Majaji wakapatikana. Siku ya shindano watu walijaa ukumbini kupita kiasi.

Bendi ya Super Matimila, chini ya Dk. Remmy ilikuwa ikitumbuiza. Hata hivyo, mitaani kote watu walijua kuwa Remmy angeibuka kuwa mshindi. Ni kwa sababu yeye mwenyewe anajinasibisha kuwa ni 'sura mbaya'. Kuna nyimbo kadhaa ambazo amejiimba mwenyewe kuwa 'Remmy mnyonge, Remmy sura mbaya', mwingine akisema 'mtoto ni mtoto hata akiwa mbaya kama Remmy ni mtoto tu.'

Kifupi hata Remmy mwenyewe umaarufu wake ulipatikana kwa staili kama hiyo. Aliingia nchini akitokea Zaire mwishoni mwa miaka ya 1970, (sasa Congo DR), akiletwa na mjomba wake Mzee Makassy. Hata hivyo alikataliwa kupanda stejini kuimba na wenzake wakidai kuwa sura yake haina mvuto, hivyo atawaharibia. Ikumbukwe kuwa Makassy ilikuwa na waimbaji watanashati sana wakati huo.

Mjomba akampa ushauri mpwa wake atunge nyimbo zake, za kuimba peke yake, ili awe anasimama jukwaani peke yake.

Hapo ndipo Remmy akatunga wimbo wa 'Siku ya Kufa', ambao uliibeba albamu nzima ya bendi hiyo na kuwa wimbo maarufu sana kuliko zote. Ni wimbo ambao pia ulianza kumpatia umaarufu sana.

Hakuchelewa, akatunga mwingine alioimba peke yake 'Harusi ya Mwanza'. Hapo ndipo kila mtu akawa anamjua Remmy. Hakugombana na mtu. Alitumia upungufu wake kujitengenezea umaarufu, akawa staa kuliko wenzake. Na baada ya hapo bado aliendelea kujipachika jina la 'sura mbaya' hata alipohamia Super Matimila.

Tukirudi kwenye shindano hilo ni kwamba jambo la ajabu lilitokea. Kijana mmoja kutoka Ilala Mchikichini, aliyejulikana kwa jina la Masudi ndiye aliyeshinda.

Hiyo ndiyo ilikuwa habari kubwa kwenye magazeti na redio wakati huo, Remmy aligaragazwa vibaya sana kwenye shindano kumtafuta mtu mwenye sura mbaya nchini.

Zawadi ilikuwa ni redio kaseti kubwa yenye spika mbili. Remmy ambaye alishika nafasi ya pili alipinga uamuzi huo wa majaji, huku mzee Jangala akikubali matokeo.

Kusema kweli Masudi ambaye baada ya hapo alipachikwa jina la Masudi Surambaya alianza kuwa maarufu kwenye vyombo vya habari kila mmoja akitaka kumfahamu mtu huyo aliyemshinda Remmy.

Kilichomuudhi zaidi Remmy ni vyombo vya habari kumwambia, pamoja na kujidai kuwa yeye ana sura mbaya, lakini mbele ya Masudi alionekana 'mrembo tu'.

Hakukubali akakata rufaa kwa majaji wa mashindano hayo, kwanza akidai kuwa Masudi hakuwa mbaya ila shida ni njaa tu ndivyo vilimfanya aonekane hivyo. Pia akaongeza kuwa mshindani mwenzake alishawahi kuugua ugonjwa na ukoma na si mbaya wa asili.

Hata hivyo, majaji baada ya kupitia ushahidi mbalimbali, waligundua jamaa hajawahi kuugua ukoma, hivyo waliitupilia mbali rufaa hiyo na kumtaka ajiande mwakani, ingawa halikufanyika kwa kukosa mdhamini.

Miaka mingi baadaye alipohojiwa, Masudi alisema maisha yake utotoni hayakuwa na furaha kwa kuwa alichukizwa na wenzake kumtania kuwa ana sura mbaya, hivyo kuwa mpweke. Lakini baada ya mashindano hayo akawa mtu maarufu, akialikwa na kushiriki matamasha mbalimbali ya wasanii na kujipatia kipato kikubwa na umaarufu pia. Alimshukuru Remmy kwa kuzidi kumuongezea umaarufu, kwani pamoja na hayo, lakini pia baadaye alikuwa akimchukua kwenye maonyesho ya bendi yake ya Super Matimila. Pia alipata kazi.

Wapo waliosema Remmy hakuwa na haja na redio, wala ushindi, na yeye tayari alikuwa staa kwenye muziki, ila alifanya hivyo ili kuzidi kufanya mashindano hayo yazidi kupata umaarufu, ingawa kwa bahati mbaya hayakuendelea.

Remmy alifariki dunia Desemba 13, 2010, Masudi naye alifariki miaka tisa baadaye siku moja tu tangu ya tarehe ya kifo cha rafiki yake Remmy, Desemba 14, 2019.

HADITHI

# HADITHI

KWANI mapenzi ni nini? Si kumpenda yule unayemtaka wewe? Kwa nini inafika wakati watu wanapangiana? Je, ukilazimisha yanaitwa mapenzi? Si yatafanana na utumwa? Yeyote anayetaka kulifanya penzi liwe na matabaka, rangi, kabila, anaweza kusababisha maafa makubwa. Donald. Kijana msomi aliyetoka nchini Marekani, anarejea nchini Tanzania. Akakabidhiwa kuendesha kampuni za baba yake. Lakini pia anatakiwa aoe. Hapo ndipo tatizo linapoanza. Usikose hata nakala moja ya riwaya hii tamu na ya kusisimua.

# Sumu ya mapenzi-9

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**

Hakupata tabu sana kupafahamu kwa kina Tausi. Aliletwa na Said jamaa wa bodaboda hadi kwenye nyumba ya kina Sadiki. Hakumfahamu jina, ila aliuliza kuwa anamuulizia msichana mmoja, akataja wajihi wake ambao aliuona kwenye picha ya video iliyopigwa na Said, akiwa na Donald, ndipo walipomwambia kuwa msichana anayemtafuta anaitwa Tausi, lakini hakai hapo. Akaelekezwa nyumbani kwao.

"Wanawake wengine bwana. hovyoo. Yaani mchumba ndiyo unanifuata kunipiga mkwara, angekuwa mume je?" Bado Tausi alizidi kumsindikiza Doroth na maneno ambayo hayo hakuyasikia, kwani gari lake lilishaanza kuondoka akiwa ameshafunga vioo.

Kwake Tausi kumuacha Donald ilikuwa ni muhali. Akifikiria maisha aliyokuwa akiishi mwanzo kabla ya kumpata mwanaume huyo na ya sasa, akili haikumpa kufanya hivyo.

Kwa sasa amekuwa mtu katika watu. Anakula anachokitaka si kinachopatikana. Anavaa nguo anayoipenda na si kwa sababu ni ya bei nafuu. Kwa sasa anaheshimika mtaani tofauti na huko nyuma. Kitendo cha Donald 'tajiri mtoto' kuja mara kwa mara na kila mtu anaona, kilimpandisha chati na kumpa heshima, akionekana ni mwanamke wa matawi ya juu mitaa yote, Magomeni Makuti.

"Atajua mwenyewe babu we. Akaroge. Akafanyaje shauri yake. Simuachi ng'o." Alijiambia mwenyewe.

******************************

Mzee Peterson alionekana kuchangayikiwa. Mkewe Eva hakuamini kile ambacho alikuwa akikisikia. "Uuuwiii. Unayoyasema haya Doroth ni kweli.?

"Ni kweli mama, nimefuatilia na nimekwenda mwenyewe na picha ndiyo hizo nimewaonyesha."

"Mimi kumpeleka Marekani kusoma, pamoja na mambo mengine ni kumfanya kupambanua kipi kizuri kipi kibaya. Mtu anarejea kutoka Marekani bado anakuwa na mambo ya kijinga namna hii." Alifoka mzee Paterson.

"Mmmh, mtoto huyu jamani,




**"Siyo hivyo tu baba Donald, wanawake wa uswahilini ni washirikina sana. Hapo unaweza kukuta tayari ameshamfanyia dawa. Unaweza kukuta baadaye hata pesa za kampuni haeleweki wapi zinapokwenda." Mama naye alidakiwa.**

yaani anakwenda kumchukua mwanamke vichohoroni huko. Si ataturudia na magonjwa huku." Eva, au mama Donald alilalamika.

"Hapa ni lazima tufanye kitu." mzee Peterson aliongea kwa sauti ya chini, lakini nzito na ya kujiamini. "Tumemsomesha, tayari tumempa kampuni aiendeshe kama Ofisa Mtendaji Mkuu. Tulikuwa tunataka sasa kumpa mke msomi, mwenye uwezo ili awe na utulivu ili apate amani moyoni, aweze kuiendesha kampuni kwa uwezo na ubunifu mkubwa wa kisasa, lakini kwa hivi anavyofanya. Kwenda kumzoa mwanamke mitaani huko uswahilini, hapo wasiwasi siyo kwa yeye tu maisha yake, hata kampuni yangu sasa inaweza kuwa kwenye mashaka, haiwezi kuendelea kukua kwa staili hii." Bado mzee Peterson aliunguruma.

"Siyo hivyo tu baba Donald, wanawake wa uswahilini ni washirikina sana. Hapo unaweza kukuta tayari ameshamfanyia dawa. Unaweza kukuta baadaye hata pesa za kampuni haeleweki wapi zinapokwenda." Mama naye alidakiwa.

Wakati huo, Doroth alikuwa kimya. Yeye mambo ya kampuni wala hakuyatilia maanani. Alichotaka ni kuokoa penzi lake ambalo sasa lilikuwa linasuasua.

Ilikuwa ni siku moja tu baada ya kutoka nyumbani kwa Tausi. Aliamua kwenda kwa wazazi wa Donald ili akawaambie kinachoendelea baina yake yeye na mtoto wao.

Ni wao ndiyo waliomtafuta na kumuona anafaa kuolewa na kijana wao. Licha ya shepu na urembo alionao, lakini elimu yake pamoja na kutoka kwenye familia ya kitajiri, vyote vilionekana kuwa ni vigezo sahihi vya kuwa na kijana wao.

Doroth alikuwa ameshakaanga mbuyu. Anaachia wenye meno watafune.

"Atekwe, halafu apelekwe sehemu akaonywe." Sauti na mzee Peterson ilisikika vema masikioni kwa Eva na Doroth. "Baba Donald, ujue tatizo si yeye. Tatizo ni mtoto wetu. Hata kama atatekwa na akaonywa. Donald ndiye anayemfuata mpaka kwao huko Magomeni Makuti. Kwa nini tusimuonye yeye huyu?"

"Sikiliza mama Donald. Ndiyo maana kwenye kikao hiki Donald hayupo. Tukimwita halafu tukamwambia hivyo anaweza kutafuta mbinu nyingine ya mawasiliano na kukutana na hicho kinyago chake. Halafu anaweza kumwambia. Donald akijua na huyo mtu wake akijua, hatutoweza tena kufanya chochote kile. Watakuwa kwenye hali ya tahadhari sana. Donald asiambiwe chochote kuhusu hili. Sisi tuamue tu nini tutafanya ili huyo msichana asiwe kikwazo tena."

"Basi baba mimi naona tukuachie wewe ufanye unachoona kinafaa." Kwa mara ya kwanza Doroth alichangia baada ya kulileta suala lile mezani. "Hayo ndiyo maneno mama. Nadhani nifunge mjadala huu. Na msimwambie chochote Donald kuhusu hili sawa?"

***********************************

Donald alipokea simu. Lakini aliyepiga alikuwa akilia.

"Nini tena mpenzi, kuna nini?"

"Kuna dada mmoja amekuja hapa nyumbani anasema eti ni mpenzi wako, kanitukana, kanitishia maisha." "Nini?"

"Kama mambo yenyewe ndiyo haya mpenzi mimi nitashindwa, mbona hukuniambia kama una mchumba?"

"Kuna mwanamke amekuja huko nyumbani kwenu?"

"Ndiyo, tena kaja na gari jeusi. Kanitukana, kanijazia watu hapa, hukuwepo lakini malaika wako walikuwepo." "Okay, nimeshamjua. Ni kweli huyo ilibidi awe mchumba wangu kabla sijakupata wewe, lakini nilipokupata nilisitisha. Naona baada ya kumueleza ukweli ndiyo akaanza kunifuatilia."

"Sasa mpenzi huoni kama hii ni hatari, mtu ananifuatilia hadi anajua nyumbani kwangu?"

"Usijali, nitaliweka sawa hili jambo." Baada ya kukata simu Donald kichwa kilimuuma. Hakutarajia kitu kama hicho mapema.


Donald sikujua kama ana mwanamke mwingine ndiyo maana alimwambia laivu kuwa hawezi kuendelea na uchumba, lakini pia kujua na kufika hadi nyumbani kwa Tausi.

Hakutarajia kwa kipindi kifupi hiki, Doroth atakuwa amefika mbali kiasi hicho.

Tayari kengele ya hatari ilianza kugonga kwenye kichwa chake. Ni kwamba jambo hili limeshafika pabaya. Na litafika hata mbele ya wazazi wake. Alijua Doroth angewaambia tu kwa sababu wao ndiyo wamemuandaa kuwa mke. Anatambua kuwa wazazi wangejua kwa sababu angewaambia yeye mwenyewe, lakini si mapema kiasi hicho. Alitaka kwanza kutengeneza mazingira.

**ITAENDELEA JUMAPILI**

## HABARI BURUDANI



# CHEMICAL AZIDI KUNOA KICHWA

HABARI njema kwa mashabiki wa rapa mkali nchini, Chemical, ambaye yupo mbioni kwenda Uingereza kusoma baada ya kupata ufadhili.

Chemical anakwenda kusoma PHD ya utafiti Scotland baada ya kupewa tuzo ya mwanafunzi bora wa tafiti wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam mwaka huu.

"Projekti yangu nilikuwa nafanya kitu ninachokipenda, nilifanyia tafiti nyimbo zinazoimbwa na wavuvi ambazo mtu akisikia anaweza akachukulia poa lakini ikashindanishwa na idara mbalimbali Chuoni lakini yangu ikawa bora" ameeleza Chemical.

## Nisher kumbe unawaona wenzio

MWONGOZAJI wa video za mwanamuziki, Nisher, amewasifu baadhi ya watu wanaofanya kazi hiyo kwa kuimarika kwao na kutengeneza video zenye ubora.

Nisher amejibu hilo baada ya kuulizwa kuhusu video zinazofanywa na waongozaji wa sasa kwenye soko la muziki kwamba zina viwango gani.

"Washikaji wa sasa hivi wanabidii, kwenye video wanaachia vitu vyenye Quality na wana njaa ni vizuri sana, wanajitahidi ila inabidi waongeze juhudi kwa sababu ubunifu bado," amesema.

Mbunge wa Jimbo la Nzega Vijijini Tabora Mhe Hamisi Kigwangalla amemsifu msanii Young Lunya na amempa moyo kwa kuendelea kufanya vizuri kwa sababu ana ujuzi mwingi.



## Young Lunya apagawa

RAPA Young Lunya, amepagawa baada ya mbunge Hamisi Kigwangalla, kujinasibu kuwa ni miongoni mwa wafuasi wake wanaomfuatilia kwa karibu.

Kigwangalla, kupitia ukurasa wake wa Twitter, ameandika kwamba kutokana na muziki mkali wa msanii huyo, hata akiwa mazoezini ngoma zake ndizo zinamvurudisha.

"Dogo Young Lunya kaupiga mwingi sana mpaka kanifanya nimfuatilie, si unajua mimi ni mpenzi wa Oldies, hawa wa kizazi chenu hawa bhana ila kani-impress sana kwa kweli! leo siku ya pili nafanya mazoezi na nyimbo zake endelea mdogo wangu," ameandika Kigwangalla.



# De Beek atakiwa kumrithi Wijnaldium

**LIVERPOOL,** England

NYOTA wa zamani wa Ajax, Sjaak Swart, amemtaja nyota wa Manchester United, Van De Beek atakuwa mrithi sahihi wa Gregion Wijnaldum pale Liverpool na atakuwa na mchango mkubwa endapo Liverpool watachukua saini ya mchezaji huyo.

Wijnaldium ameondoka Liverpool kama mchezaji huru na anatajwa kujiunga na Barcelona kule Katalunya.

Van De Beek alisajiliwa na United Septemba, mwaka jana kwa dau la euro milioni 35 na hadi sasa ameanza katika mechi nne tu, huku akitokea benchi katika mechi 36 na kufanikiwa kufunga bao moja na pasi moja ya mwisho.

Swart anadai Van De Beek alikuwa anacheza vyema pale Ajax kabla yakwenda United, lakini wingi wa viungo umelazimisha apate nafasi finyu ya kucheza.

"Hajawa na wakati mzuri wa kucheza, lakini akipata klabu nzuri basi bila shaka atang'aa zaidi," amesema Swart akinukuliwa na BT Sport.

"Anaweza kuwa na nafasi Liverpool na atakuwa mrithi sahihi wa Wijnaldum na atapa nafasi nafasi nyingi ya kucheza."

"Klabu kama Liverpool au Bayern Munich zinaweza kuwa sehemu sahihi sana kwa ajili ya mchezaji huyu na kuondoka kwa Wijnaldum klabuni hapo kunaweza kuwa nafasi ya Van De Beek Kung'aa."





# DE BRUYNE SHAKANI KUIVAA URUSI

**BRUSSLES,** Ubelgiji

KEVIN De Bruyne huenda akakosa mechi ya ufunguzi ya Ubelgiji kwenye michuano ya Euro 2020 dhidi ya Urusi itakayochezwa Juni 12, mwaka huu, amesema Kocha, Roberto Martinez.

De Bruyne ni majeruhi baada ya kuumia usoni katika harakati za kuwania mpira dhidi ya beki wa Chelsea, Antonio Rudiger, kwenye mechi ya fainali za Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Manchester City iliyochezwa mwishoni mwa wiki iliyopita.

Kiungo huyo hajatakiwa kufanyiwa upasuaji, lakini Martinez hana hakika kama mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 29 atakuwa tayari.

Kama De Bruyne hatarejea uwanjani, bosi huyo wa Ubelgiji amethibitisha atavaa 'mask' kama inayovaliwa na Jan Vertonghen baada ya kuumia akiichezea Tottenham miaka miwili iliyopita.

Kevin De Bruyne alivunjika pua na kupata hitilafu kwenye jicho.

Akizungumza mapema wiki hii, Martinez alisema De Bruyne hahitaji upasuaji.

"De Bruyne anaonekana atakuwa fiti kwa mechi ya kwanza na kama atakuwa na mbadala nitasema."

"Tumefanya uamuzi kuhusu mask yake, itakuwa kama ile ya Jan Vertonghen."

"Nitasema wiki ijayo, hatujui kwa hakika tutakuwa vipi na Kevin kwa sasa mwacheni apumzike."

# England hatihati kumkosa -Arnold

**LONDON,** England

KOCHA Mkuu wa Timu ya Taifa ya England, Gareth Southgate, amesema Trent Alexander-Arnold anaweza kukosa michuano ya Euro 2020 kutokana na kuwa majeruhi.

Alexander-Arnold alilazimika kutolewa nje ya dimba mwishoni mwa mchezo wa England wa ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Austria pale Middlesbrough Jumatano jioni, na kuweka mashaka juu ya ushiriki wake kwenye mashindano ya Euro 2020.

Na sasa Southgate amesema kuna uwezekano nyota huyo akaikosa michuano hiyo baada ya kuumia paja.

Southgate alichagua kikosi cha kwanza cha wachezaji 11 cha majaribio, na Tyrone Mings na Conor Coady wote wakianza nafasi ya beki, pamoja na beki wa kulia wa Liverpool na Kieran Trippier wa Atletico Madrid.

Jude Bellingham, Jack Grealish na Declan Rice pia walianza, vile vile Harry Kane na Jesse Lingard.

Jeraha la Alexander-Arnold, limekuja siku moja tu baada ya kikosi kutangazwa.

Mchezo wa kwanza wa England kwenye Euro 2020 ni dhidi ya Croatia utakuwa mwezi Juni 13, mwaka huu.



# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# MADRID YATANGAZA KUTOMUUZA HAZARD

Uamuzi huo umefikiwa baada ya Kocha Ancelotti kutua klabuni hapo akichukua mikoba...

**MADRID,** HISPANIA

NYOTA wa Real Madrid, Eden Hazard na Gareth Bale hawatauzwa baada ya Carlo Ancelotti kutangazwa kuwa kocha mpya wa timu hiyo kuelekea msimu ujao.

**Hazard amekuwa na maisha magumu kwenye viunga vya Bernabeu tangu atue akitokea Chelsea mwaka 2019 kwa dau la pauni milioni 103.**

Amekuwa akisumbuliwa na majeraha ya mara kwa mara yanayomfanya asicheze mechi nyingi za kimashindano, jambo linaloshusha sana kiwango chake.

Baada ya Ancelotti kutangazwa kuwa kocha wa Madrid, Hazard alifanya mahojiano na RTBF na alipoulizwa kuhusu suala hilo akasema: "Kila mmoja kwenye timu anajua Ancelotti aliwahi kuwapo hapa, hapo kabla na akashinda taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya. Anawafahamu wachezaji wengi waliopo kikosini kwa sasa.

"Hata sisi tunajua kwamba ana uzoefu mkubwa, anawajua mashabiki wa Madrid na hata mazingira ya mji, nina uhakika tutafanya mambo makubwa kupitia yeye.

"Simjui kiundani sana, lakini kwa kile nilichokisikia ni kwamba yeye ni mtu mzuri ambaye kila siku anahitaji kushinda tu jambo ambalo kila mtu analihitaji. Kufanya naye kazi sehemu moja ni jambo zuri kwangu."

Kwa upande wake Ancelotti alipoulizwa kuhusu Hazard alisema: "Ni mchezaji mzuri, amekua na matatizo ya majeraha lakini hiyo haionekani kumwondoa kwenye ubora wake kwa sababu ana shauku ya kufanya vizuri siku hadi siku.

"Gareth naye hakucheza sana kwenye ligi lakini alifanikiwa kufunga mabao. Alikuwa na mchango mkubwa kwenye mechi za mwisho ambapo alicheza kwa kiwango cha juu sana. Namfahamu vizuri. Kama atapewa motisha ya kutosha, anaweza kuwa na msimu mzuri. Sina shaka na hilo."

Hazard pia alieleza kuhusu kocha wake wa zamani Zinedine Zidane ambaye aliondoka mara baada ya msimu uliopita kumalizika bila ya Madrid kushinda taji lolote.

Msimu uliopita, Hazard alianza kwenye michezo 14 tu ya La Liga na akafunga bao moja na kutoa asisti tatu tu.

Real ilitegemea kupata kitu kikubwa zaidi kutoka kwa fundi huyo iliyomsajili kama Galactico lakini hakulifanya hilo.

## ZISIKUPITE

### PIRLO, SARRI WACHUANA

ANDREA Pirlo na kocha wa zamani wa Chelsea, Maurizio Sarri wote wanatajwa kuwaniwa na Everton. ***(Calciomercato via Liverpool Echo)***

### VILLA YAMBANIA GREALISH

KIUNGO wa Aston Villa na England, Jack Grealish (25), anaweza kubakia klabuni hapo kipindi hiki cha majira ya joto, baada ya Manchester City na Manchester United kutokuwa tayari kulipa ada ya pauni milioni 130 inayotakiwa na klabu ya nyota huyo. ***(Talksport)***

### FERNANDINHO KUTEMWA

KIUNGO wa Manchester City na Brazil, Fernandinho mwenye umri wa miaka 36, na straika wa Newcastle na England, Andy Carroll (32), wote wamejumuishwa kwenye orodha ya kuachwa na klabu zao. ***(Premier League)***

### 'POGBA' ANUKIA CITY

MANCHESTER City inakaribia kumsajili kiungo wa Fluminense, Metinho mwenye umri wa miaka 18, ambaye anajulikana kama 'Paul Pogba' wa Brazil. ***(Goal)***

### ZIYECHI AWEKWA SOKONI

CHELSEA haijaondoa uwezekano wa kumuuza winga wa Morocco, Hakim Ziyech kipindi hiki cha majira ya joto, huku miamba wa Serie A, AC Milan na Napoli zote zinamwania mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28. ***(Calciomercato)***

### MILAN YAMTAKA TOMORI

AC Milan imeiambia Chelsea inataka kumsajili kwa mkataba wa kudumu mlinzi wa kati, Fikayo Tomori mwenye umri wa miaka 23, ambaye thamani yake ni pauni milioni 28.5. ***(Fabrizio Romano)***

### ANCELOTTI AWAAMSHA NYOTA

WACHEZAJI wa Everton walipatwa na mshituko walipogundua kwamba Carlo Ancelotti anarudi Real Madrid, huku fowadi wa Brazil, Richarlison mwenye umri wa miaka 24, na nyota wa Colombia, James Rodriguez (29), wote wanafikiria kuhusu majaliwa yao. ***(The Athletic - subscription required)***

### BUENDIA ANUKIA ARSENAL

ARSENAL inapanga kumsajili kiungo wa Norwich, Emi Buendia mwenye umri wa miaka 24. ***(Times - subscription required)***

### ARTETA AMTAKA DEMBELE

KOCHA wa Arsenal, Mikel Arteta anawania kumsajili straika wa Lyon, Moussa Dembele mwenye umri wa miaka 24. ***(Telegraph)***

### BAYERN KUMSAJILI NIGUEZ

BAYERN Munich inapanga kumsajili kiungo wa Atletico Madrid na Hispania, Saul Niguez mwenye umri wa miaka 26, kwa euro milioni 80. ***(Radio Marca)***

HABARI MICHEZO

## Mtibwa Sugar yasaka pointi 6

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Mtibwa Sugar, Mohammed Badru amesema anahitaji pointi sita ili kupata uhakika wa kubakia Ligi Kuu Tanzania Bara katika msimu ujao.

Badru aliliambia gazeti hili jana malengo yao makubwa ni kuhakikisha wanapata ushindi kwenye michezo minne zilizobakia au mbili na kujitoa kwenye hatari ya kushuka daraja na kibarua hicho kitaanzia dhidi ya Mwadui FC na KMC FC.

"Mipango yangu ni kushinda mechi mbili za mwanzo, tumejiandaa kwenda kushinda na baadaye twenda kutafuta pointi tatu zingine dhidi ya KMC FC na imani na wachezaji wangu kupata alama hizo na kuinusuru timu na msimu ujao kuendelea kuwapo katika ligi hii," alisema Badru.

Kocha huyo alisema wakifanikiwa kuondoka na pointi hizo sita au zaidi watafikisha pointi 40 na kujiondoka katika nafasi ya 11 ambayo si salama kwa sasa.

"Ligi iko ukingoni hivyo lazima kila timu zijipange vizuri kwa upande wangu natamani kupata pointi 12 katika michezo minne iliyobakia ila hata wapinzani wetu nao wamejipanga kupata matokeo mazuri hivyo kwangu sita za mechi mbili za kwanza," alisema Badru.

Mtibwa Sugar imebakiza mechi nne ambazo zote watacheza ugenini dhidi ya Mwadui FC (Kambarage, Shinyanga), KMC FC (Uhuru- Dar es Salaam) na Dodoma Jiji FC na mwisho watamaliza msimu na JKT Tanzania kwenye Uwanja wa Jamhuri jijini Dodoma).

## Mabeki watajwa kuivuruga JKT TZ

**Na Adam Fungamwango**

IKIWA kwenye hatari ya kushuka daraja, benchi la ufundi la JKT Tanzania imesema matokeo mabaya ambayo wamepata katika mechi mbalimbali msimu huu yamesababishwa na safu ya ulinzi kuwa dhaifu.

Kocha Msaidizi wa JKT Tanzania, Amos Mgisa alisema safu ya ulinzi ya timu hiyo ilikuwa inafanya makosa mengi yaliyowapa wapinzani faida na hivyo kujiweka kwenye nafasi ya hatari.

"Mwenendo wetu msimu huu haukuwa mzuri sana. Umetokana na matatizo kwenye safu yetu ya ulinzi. Imekuwa ikifanya makosa mengi sana yaliyosababisha tupoteze mechi au tufungwe mabao mengi," alisema Mgisa, straika wa zamani wa timu hiyo wakati huo ikiitwa JKT Ruvu.

Mgisa alisema wamekuwa wakirekebisha makosa hayo na kwa kipindi hiki cha mapumziko ya mechi za Ligi Kuu, wameanza kuisuka beki yao ili isiendelee kufanya makosa zaidi katika michezo iliyosalia.

Naye mchezaji wa timu hiyo, Nurdin Mohamed, alisema wao kama wachezaji watajitahidi kwa kila hali kuhakikisha wanaibakisha JKT kwenye Ligi Kuu Bara.

# UCHAGUZI NAFASI YA RAIS ZFF MAMBO HADHARANI

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

SHIRIKISHO la Soka Zanzibar( ZFF), linatarajia kufanya uchaguzi wa kujaza nafasi ya Rais ifikapo Juni 27, mwaka huu imeelezwa.

**Uchaguzi huo unafanyika kufuatia Rais aliyekuwa madarakani, Seif Kombo Pandu, kutangaza kujiuzulu katika nafasi hiyo mapema Februari, mwaka huu.**

Akizungumza na gazeti hili jana, Mwenyekiti wa Kamati ya Uchaguzi ya shirikisho hilo, Fadhili Ramadhani Mberwa, alisema mchakato wa kuchukua fomu kwa wadau wanaotaka kuwania nafasi hiyo ya juu ulianza rasmi Juni 3, mwaka huu na unatarajiwa kumalizika ifikapo keshokutwa.

Mberwa alisema usaili kwa wagombea wote watakaokuwa wamerudisha fomu utafanyika Juni 13, mwaka huu na kamati yake itaanza kupokea pingamizi kuanzia siku hiyo hadi Juni 18, mwaka huu.

Kiongozi huyo alisema kamati yake imepangwa kusikiliza pingamizi ifikapo Juni 20, mwaka huu na hilo litafanyika endapo watakuwa wamepokea pingamizi hizo kutoka kwa wadau mbalimbali.

"Kwa mujibu wa kalenda yetu, Juni 20 pia itakuwa ni siku ambao wagombea wanaruhusiwa kuanza kampeni kuelekea uchaguzi huo na mwisho wake utakuwa ni saa 6:00 usiku siku ya Juni 26," alisema Mberwa.

Alitaja sifa za mgombea wa nafasi hiyo elimu ngazi ya Shahada ya Kwanza, awe Mzanzibari na awe na uzoefu katika maswala ya mpira wa miguu usiopungua miaka mitano.

Alisema pia mgombea anatakiwa awe na umri wa miaka kuanzia 25 hadi 65 na kuongeza fomu za kuwania nafasi hiyo ya uongozi zinatolewa katika Ofisi za ZFF zilipo kwenye Uwanja wa Amaan pamoja na ile iliyopo Gombani Kisiwani Pemba.

Mwenyekiti huyo amewataka wadau wa mpira wa miguu Zanzibar kujitokeza kwa wingi kuchukua fomu za kugombea nafasi hiyo pomoja na kufanya kampeni za kistaarabu pale muda utakaporuhusu ili kukamilisha mchakato huo kwa amani.

Wakati huo huo, Bodi ya Ligi Kuu Zanzibar (ZBL), imesema michezo ya kufunga pazia la msimu 2020/21 yote itafanyika siku moja ili kuepusha upangaji wa matokeo.

Mjumbe wa ZBL, Mohamed Masoud alisema mabadiliko hayo ya ratiba yamefanyika ili kuepuka upangaji wa matokeo na kwenye upande wa timu zinazotaka kushuka daraja.

Masoud alisema bodi ya ligi hiyo itakutana kupanga tarehe mpya ya siku ya kumaliza msimu ambapo timu nyingine moja itaungana na Hard Rock katika kushuka daraja.



Wanafunzi wa Shule ya Msingi ya Al- Hekma wakishindana kuvuta kamba katika Tamasha la Wiki ya Mtoto wa Azam lililofanyika kwenye Uwanja wa Azam Complex jijini Dar es Salaam jana. Shule tatu za msingi za jijini hapa zimeshiriki tamasha hilo. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# *Gaguti aitabiria makubwa Mtwara*

**Na Abdallah Khamis,** MTWARA

MKUU wa Mkoa wa Mtwara, Brigedia Jenerali Marco Gaguti, ametaja mambo manne yatakayoufanya mkoa huo katika mashindano ya Umoja wa Michezo kwa Shule za Msingi Nchini (Umitashumta), na ya Sekondari (Umiseta) yatakayofanyika kuanzia keshokutwa.

Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, ndiye anatarajiwa kuwa mgeni rasmi katika uzinduzi wa michuano hiyo.

Brigedia Gaguti ameyataja mambo hayo kuwa ni wenyeji wa mashindano, kambi bora ya muda mrefu, walimu makini na wazoefu katika nyanja za michezo pamoja na kuungwa mkono na wakazi wa mkoa huo.

"Mikoa wageni wajipange kisawa sawa, tumedhamiria kushinda na tutashinda kweli kwa kuwa tuna sababu nyingi za kufanya hivyo," alisema Brigedia Jenerali Gaguti baada ya kutembelea kambi ya timu za Mtwara.

Gaguti alisema maandalizi ya michezo yamekamilika na wanamichezo 7,440 watashiriki michezo hiyo ambayo upande wa Umitashumta itaanza Juni 8 hadi 19, mwaka huu huku Umiseta ikitarajiwa kuchezwa kati ya Juni 19 hadi Julai 3, mwaka huu.

Naye Leonard Thadeo, Mratibu wa michezo hiyo kutoka Ofisi ya Rais Tamisemi amesema wameridhishwa na maandalizi yaliyofanyika na kilichobaki ni washiriki kuonyesha vipaji vyao walivyojaaliwa.

"Katika michezo ya aina hii kumeshapatikana vipaji vingi vilivyofanya vizuri katika michezo mbalimbali kwenye ngazi ya Taifa na Kimataifa, sasa ninatarajia kuona vipaji vingine vikijitokeza hapa." alisema Thadeo.

# Michezo

Jumapili Juni 6 , 2021

Nipashe





Madrid yatangaza kutomuuza Hazard UKURASA 22




Kiungo wa Yanga, Deus Kaseke (kushoto), akijiandaa kumtoka beki wa timu hiyo, Kibwana Shomari, katika mazoezi ya kujiandaa na mechi zilizosalia za Ligi Kuu Tazania Bara msimu wa 2020/21 pamoja na mchezo wa nusu fainali ya michuano ya Kombe la FA watakaocheza dhidi ya Biashara United. **PICHA: MTANDAO**

## Kahata aishukuru Simba SC 'imemnadi'

**Na Saada Akida**

WAKATI uongozi wa Azam FC ukisema hawana mpango wa kumsajili aliyekuwa kiungo wa mabingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara Simba, Francis Kahata, nyota huyo raia wa Kenya ameshukuru kwa muda wote aliokuwa kwenye kikosi hicho cha Wekundu wa Msimbazi.

Kahata alisema ndani ya kikosi cha Simba alikuwa na safari ndefu, tamu, isiyokumbukwa na yenye uchungu tangu alipofika hapa nchini.

"Nilipokea msaada mkubwa na upendo kutoka kwa timu ya watendaji iliyoongozwa na Mohammed Dewji (Mo), wafanyakazi wa benchi la ufundi, wachezaji na mashabiki wa Simba, shukrani zangu zimwendee Kocha Mkuu, Didier Gomes kwa nafasi ya kuwakilisha rangi nyekundu na msaada mzuri na kila mtu aliyekuwa na njia moja na mimi."

"Ninaondoka nikiwa nimeinua kichwa juu na kujivunia mafanikio yangu kwenye klabu, imefika wakati wa kuaga na kuwaaga nyote, mwanamume anapaswa kutafuta changamoto mpya na kushukuru kwa kila kitu nilichopata kwenye timu, ninawatakia kila la kheri katika msimu ujao,... miaka miwili ilistahili," alisema Kahata.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Azam FC, Abdulkarim Amin 'Popat' aliliambia gazeti hili klabu yao haina mpango wa kumsajili Kahata ambaye kwa sasa ni mchezaji huru.

"Suala la Kahata, hapana sio ukweli ni tetesi kwa sababu bado hatujakaa na kocha (George Lwandamina), kwa sasa tunawaongeza mikataba wachezaji wetu ambao mwalimu amewahitaji ila kuhusu nyota kutoka nje bado tunasubiri ligi imalizike," alisema Popat.

# Yanga yaweka mikakati mezani

**Saada Akida na Adam Fungamwango**

### ●●● Yaahidi itakamilisha 'jambo lao' na kufikia malengo yao ya msimu huu huku ikijiimarisha kuelekea...

WAKATI uongozi wa Yanga ukiwataka mashabiki na wanachama wa timu hiyo kutokuwa na presha wakati huu Ligi Kuu Tanzania Bara ikielekea ukingoni, nyota wa zamani wa klabu hiyo wameishauri Kamati ya Usajili kusajili mastraika wenye ubora kwa ajili ya msimu ujao ili wacheze soka la ushindani.

**Akizungumza na gazeti hili jana, Kaimu Katibu Mkuu wa Yanga, Haji Mfikirwa, alisema klabu hiyo imejipanga vizuri kuhakikisha wanashinda mechi zao tano zilizobakia msimu huu pamoja na kubeba ubingwa wa mashindano ya Kombe la FA.**

Mfikirwa alisema bado hawajakata tamaa katika mapambano ya kuwania ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara ambalo ndio lengo kuu na ili kufikia huko wanahitaji kupambana hadi siku ya mwisho ya kumalizika kwa msimu huu.

Katibu huyo alisema mipango yao ni kuhakikisha wanamaliza msimu bila kupoteza mechi yoyote lakini pia kupata matokeo mazuri katika mchezo wao wa hatua ya nusu fainali ya Kombe la FA dhidi ya Biashara United kutoka mkoani Musoma.

"Kocha Nabi (Nesreddine) ameweka mipango yake kuelekea mechi hizo tano za ligi, pamoja na mchezo wetu wa nusu fainali ya FA ili kuhakikisha tunacheza fainali na kutwaa ubingwa ambao utatufanya kushiriki katika michuano ya kimataifa msimu ujao," alisema Mfikirwa.

Aliongeza wachezaji wao wako kambini na wanaendelea vizuri na mazoezi kwa sababu wanafahamu wana jukumu zito mbele.

Katibu huyo alisema wanachokifanya kwa sasa ni kuhakikisha timu yao itapata ushindi katika kila mechi huku wakiacha kufuatilia matokeo ya wapinzani wao hasa Simba ambao wanaongoza kwenye msimamo wa ligi.

Bakari Malima 'Jembe Ulaya' ambaye aliwahi kuichezea timu hiyo aliweka wazi kwamba eneo la ushambuliaji ndilo limewaangusha zaidi msimu huu.

Jembe Ulaya alisema wanasikitisha kuona hakuna mcheza yoyote wa Yanga ambaye yuko kwenye kinyang'anyiro cha kuwania ufungaji bora.

"Yanga wanatakiwa kuongeza watu wengine kwenye uwezo wa kupachika mabao. Kuna matatizo sana sehemu ya ushambuliaji, ingawa katikati kidogo kunatakiwa kufanyiwa marekebisho, lakini mbele ni matatizo," alisema Jembe Ulaya.

Naye Ramadhani Kampira alishauri Ligi Kuu Tanzania Bara itakapomalizika, suala ya usajili liwahusishe wajumbe wengi, hasa wachezaji wa waliowahi kuichezea timu hiyo ili kupata wachezaji wapya wenye uwezo mkubwa wa kuichezea timu kama hiyo.

"Yanga ilifanya kosa kubwa sana kumwachia David Molinga. Yule ndiyo alionekana kama mzito hivi kwa sababu hajacheza muda mrefu, lakini alikuwa ni mshambuliaji mzuri sana kama angepewa muda, sema mihemko ya mashabiki ikawaingia viongozi wakaachana naye. Hata kama hawatowaondoa mastraika waliopo, lakini watafute wengine," alisema Kampira.

Aliongeza kama viongozi wake wataendelea kufanya usajili kwa mfumo ule ule, watarajie hali ya kusuasua itajirudia.

"Mimi nawashauri watoe nafasi kwa wachezaji wa zamani ndiyo watafute wachezaji. Kuna wachezaji wazuri Zambia, Congo DR, lakini nani anakwenda kuwaangalia na kuwaleta. Bado sisi Yanga tuna tatizo kwenye ushambuliaji, hilo ndiyo kwanza lingekuwa kipaumbele kuliko mengine," alisema winga huyo wa zamani.

Katika msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Yanga iko katika nafasi ya pili ikiwa na pointi 61 na imebakiza mechi tano ili kumaliza msimu ambazo ni dhidi ya Ruvu Ruvu Shooting itakayochezwa Juni 17, Mwadui FC (Juni 20), Simba (Julai 3), Ihefu (Julai 14) na itafunga pazia kwa kuwafuata Dodoma Jiji FC kwenye Uwanja wa Jamhuri jijini Dodoma hapo Julai 18, mwaka huu.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >